**KIKWETE** aonya viongozi Afrika kuhusu ubinafsi

UKURASA 2



**MAPAGALE** yatajwa maficho ukatili wa kijinsia watoto Z'bar

UKURASA 17


'Cheti cha ndoa hakisainiwi wakati wa uchumba'
Ukurasa 13
Kariakoo 'kuchele' ni mambo yanayojiri baada mkutano wa Waziri Mkuu Majaliwa
Ukurasa 12
BUFE
IJUMAA JULAI 21, 2023
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

Vyanzo vuta nikuvute, kushindwa kurejesha mikopo kumbe viko hapa

Na Christina Haule, MOROGORO

MIGOGORO kati ya wakopaji na taasisi za fedha zinazokopesha inazidi kukua kila siku, huku visa vyake vikiwa kutozwa riba kubwa, kufilisiwa, kuvunjika kwa ndoa kwa upande mmoja na hasara kwa taasisi baada ya aliyekopa kuingia mitini, vikisikika mara kwa mara.

Aidha, wakopaji mikopo kushindwa kulipa hasa baadhi ya kinamama wajasiriamali ni jambo linaloshika kasi huku baadhi yao wakitokomea kusikojulikana na kuziachia hasara taasisi zinazotoa mikopo na hata familia zao.

Haya yanatokea licha ya kuwapa elimu na mbinu za kutumia kwa tija pesa hizo wanazokopa ili kukuza mtaji au kuboresha biashara...

...waliyonayo, bado changamoto hiyo imeendelea kushika kasi.

Kadhalika, anawashauri wajasiriamali kuzingatia elimu wanazopewa hasa za masuala ya mikopo ili kutojiingiza kwenye mikopo umiza ambayo ina mchango mkubwa wa kuwaharibia maisha na uwekezaji kwa sababu ya kukimbia na kuacha shughuli za maendeleo wanazofanya, ili kujiepushia matatizo.

Halikadhalika, Ntambi anasisitiza taasisi nyingine za kifedha kutumia mfumo wa taarifa za wakopaji mikopo uliopo serikali (credit bureau) katika kuweka maelezo ya wateja wa mikopo na kusaidia watoa huduma wengine kuwatambua na kutowapa fedha nyingine...

UKURASA 11


Ijumaa Julai 21, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581378

www.ippmedia.com



www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


# Kikokotoo mafao chazua kilio polisi

**TUME** ya Haki Jinai yabaini wastaafu kupunjwa stahiki, Magereza nako...*Endelea ukurasa wa 2*

UKURASA WA 7

### TAWA YABAINI MBINU TATU MPYA MAJANGILI WA TEMBO

MAMLAKA ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA) imebaini mbinu tatu mpya zinazotumiwa na majangili wa tembo kukwepa kukamatwa, ikiwamo kuyawekea kemikali meno ya wanyamapori...



UKURASA WA 8

VITA DHIDI YA AJALI BARABARANI

### KAMPUNI YAFADHILI MAFUNZO KWA POLISI

KAMPUNI ya Superdoll imeguswa na kauli ya Rais Samia Suluhu Hassan dhidi ya ajali za barabarani zinazogharimu maisha ya watu. Imefadhili mafunzo maalum kwa polisi kukabiliana na ajali hizo....



UKURASA WA 19

### UJENZI VITUO VYA GESI ASILIA KWA AJILI YA MAGARI WAIVA TPDC

SHIRIKA la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), liko katika hatua za mwisho kuanza ujenzi wa kituo kikuu cha kujaza gesi asilia kwenye magari na kwa matumizi ya...



Mmoja wa watuhumiwa wa utapeli wa simu za wanafunzi wanaosoma masomo ya ziada Mwenge wilayani Kinondoni, Dar es Salaam, akiomba msamaha asipigwe na madereva wa bodaboda baada ya kukamatwa katika eneo hilo jana. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**





## Mpango ashtuka maambukizi VVU, unyonyeshaji duni

UKURASA 3

# Askofu amnasa frateli feki kanisani

UKURASA 3

**MICHEZO** **YANGA: TUTATETEMESHA NCHI** UK. 24 **KATUNI** UK. 6



Wananchi wakipatiwa maelezo katika Banda la Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere kwenye Maonesho ya 18 ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia (TCU), yanayoendelea Viwanja vya Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Kikokotoo mafao chazua kilio

**Na Waandishi Wetu**

TUME ya Kuangalia Jinsi ya Kuboresha Taasisi za Haki Jinai nchini, imebaini malalamiko makubwa kwa askari wa Jeshi la Magereza na Jeshi la Polisi wa vyeo vya chini kuhusu mafao ya uzeeni, wakidai kupunjwa kutokana na mishahara midogo, huku ikipendekeza kuwe na mabadiliko makubwa.

Ripoti hiyo iliyokabidhiwa kwa Rais Samia Suluhu Hassan wiki iliyopita, ilibaini hali mbaya kwa askari wengi katika malipo ya mafao ya mkupuo ya kustaafu katika ziara zilizofanyika, hasa kwa askari wa vyeo vya chini kutokana na kustaafu katika umri mdogo.

"Msingi wa malalamiko hayo ni kuwa, utaratibu mpya wa kukokotoa mafao ya mkupuo umeathiri kwa kiasi kikubwa kiwango cha malipo hayo kutokana na malipo yao kuhusisha posho nyingi na umri wa kustaafu kuwa mdogo, hivyo kusababisha askari kulipwa kiasi cha fedha ambacho hakikidhi mahitaji," inabainisha sehemu ya ripoti hiyo.

Tume hiyo pia imependekeza mishahara ya askari wa Jeshi la Polisi na Jeshi la Magereza iboreshwe kwa posho za msingi za kisheria kujumuishwa katika mishahara yao ili kuwawezesha kupata mafao ya mkupuo yanayoridhisha wakati wa kustaafu.

Akifafanua ripoti hiyo kwa wahariri wa vyombo vya habari jana Ikulu, jijini Dar es Salaam, Mjumbe wa tume hiyo, Dk. Laurean Ndumbaro, alisema askari wana posho nyingi na inawezekana posho hiyo kufikia Sh. milioni 1.9 ila mshahara ni Sh. 900,000 kwa mwezi, hivyo askari akipigiwa hesabu ya kikokotoo kiwango kinakuwa kidogo.

"Tumeshauri posho zijumuishwe katika mshahara ili ziwe nyingi na akikatwa na wakati wa kustaafu akipigiwa hesabu angalau anapata mkupuo unaofaa,"alisema Dk. Ndumbaro ambaye ni Katibu Mkuu Utumishi.

Mjumbe mwingine wa tume hiyo, Balozi Ernest Mangu, ambaye aliwahi kuwa Mkuu wa Jeshi la Polisi, alisema tatizo kubwa ni askari polisi kulitumikia jeshi hilo kwa muda mfupi, hivyo uchangiaji wao katika mifuko ya hifadhi ya jamii tofauti na wale wa vyeo vya juu wanaowajibika hadi miaka 60 na kupata mafao yenye unafuu.

Ripoti ya tume hiyo inapendekeza umri wa kustaafu kwa askari wenye vyeo vya chini katika Jeshi la Polisi na Jeshi la Magereza uongezwe na kuoanishwa na ule wa watumishi wa umma, ili muda wa kuchangia katika mfuko wa pensheni uongezeke.

Kwa sasa umri wa askari polisi kustaafu ni miaka 50-55.

**UTASHI KISIASA**

Makamu Mwenyekiti wa Tume hiyo, Balozi Ombeni Sefue, aliwaambia wahariri jana kuwa wana imani mapendekezo yao yatatekelezwa kutokana na utashi wa kisiasa wa Rais Samia.

"Tulikopita kote wananchi walituuliza 'tume hii ina tofauti gani na zingine zilizokuja kutuhoji?' Tuliwaambia utashi wa kisiasa wa Rais Samia ni mkubwa sana.

"Sisi tuliopata nafasi ya kukaa naye karibu tunaona kabisa. Alitaka wananchi washirikishwe na ndio maana tumetembea mikoa yote na kuyafikia makundi yote," alisema.

**MA-DC, MA-RC**

Balozi Sefue alisema suala la wakuu wa wilaya kujichukulia madaraka, ikiwamo kuwakamata watu limelalamikiwa.

"Kuna sehemu mtu amesema DC 'anammendea' msichana wake, anasweka ndani Ijumaa, hautoki mpaka Jumatatu. Tunachosema yale mamlaka waliyopewa wakuu wa mikoa na wa wilaya yalikuwa na sababu. Tatizo si wao kuwa na mamlaka, tatizo yametumika vibaya," alifafanua Balozi Sefue.

Alisema viongozi hao kila wakati wanatembea na vyombo vya dola ilhali wengine hawajui sheria inayowaruhusu kukamata huku mashauri mengi yakiishia njiani.

**UTITIRI WA MAJESHI**

Balozi Sefue pia alisema wamependekeza askari wanaoshughulika na kupambana na majangili wavae sare za jeshi na kubeba silaha tofauti na ilivyo sasa.

"Tulipokuwa tunazunguka kupata maoni ya wananchi tuliulizwa 'hivi tuna serikali ngapi?' Nikamuuliza 'kwanini?' Akaniambia anachokijua jeshi lipo moja ila ukiamka asubuhi hujui utakamatwa na jeshi lipi. Utakamatwa na polisi, TAKUKURU, watu wa misitu na watu wa wanyamapori," alisema.

Mjumbe wa tume hiyo ambaye ni Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Eliezer Felishi, alisema ukamataji wa wahalifu unatakiwa utolewe taarifa kituo cha polisi.

Alisema kuna udhaifu umeonekana katika ukamataji kwa kuwa kuna wakati mtu anakamatwa bila kituo cha polisi kilichoko jirani kupatiwa taarifa huku baadhi ya wakuu wa wilaya na mikoa wakikamata watu bila kuwafikisha mahakamani au kufuata sheria.

Omari Issa, mjumbe wa tume hiyo, alitaja maeneo matatu ambayo yanapaswa kuzingatiwa; utii wa sheria, kutenda haki na kutoa huduma zinazotakiwa.

Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais Ikulu, Zuhura Yunus, alisema Rais Samia ameipa haki kipaumbele na ndiyo maana tangu aingie madarakani, zaidi ya mahabusu 2,240 wameachiwa.

Alisema lengo la Rais Samia ni kushughulikia malalamiko ya muda mrefu ya wananchi kuhusu utoaji wa haki tangu alipoingia madarakani.

# Kikwete aonya viongozi Afrika ubinafsi

**Na Gwamaka Alipipi**

RAIS mstaafu, Jakaya Kikwete amewataka viongozi wa Afrika kutokuwa wabinafsi, akiwataka wajitoe kusaidia wananchi kama njia ya kukumbuka maisha, maono ya Rais wa zamani wa Afrika Kusini, Nelson Mandela.

Amesema Mandela alipokuwa Rais wa Afrika Kusini alikuwa ni mtu wa kawaida, mpole asiyependa cheo chake kimkandamize mwingine, hata mavazi aliyovaa yalikuwa ya kawaida.

Aliyasema hayo jana katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), wakati akitoa mada iliyohusu kumbukumbu ya miaka 10 ya kifo cha Nelson Mandela.

Alisema Mandela ni alama inayoishi miaka na miaka kwa sababu maisha aliyoishi yaliwajali wananchi, alichukia uonevu, dhuluma.

"Alikuwa ni mtu wa kipekee sana, asiyependa kutukuzwa, msema kweli, hata alipokuwa anaumwa aliwaeleza wananchi kwamba anasumbuliwa na ugonjwa wa saratani. Nelson Mandela alikuwa mtu wa kipekee sana," alisema Kikwete.

Kikwete alisema Mandela ndiye shujaa wake katika maisha na kiongozi aliyekuwa na roho ya kusamehe kwa wale waliomkosea, kumfunga miaka 27 gerezani.

**AELEZA ALIVYOKUTANA NAYE**

Kadhalika, Kikwete alisema mara ya kwanza kukutana na Mandela na kuzungumza naye (yeye) alikuwa ni Waziri wa Madini, ilikuwa ni kwenye mkutano wa mawaziri wa sekta ya madini uliofanyika Afrika Kusini.

Alisema wakati wa mkutano huo Mandela hakuwa rais bali alikuwa ametoka kutumikia kifungo gerezani na alikuwa mgeni rasmi wakati wa kufunga.

Kikwete alisema baada ya mkutano huo, Mandela aliwaalika mawaziri wote katika hafla ya chakula cha jioni, hapo ndipo alipopata nafasi ya kuzungumza naye na kumfahamu zaidi ni mtu wa namna gani.

"Ilikuwa ni furaha kwake kukutana na shujaa, kuongea naye ilikuwa ni fahari sana kwangu. Nilipokuwa Waziri wa Mambo ya Nje, nilipata fursa nyingi sana ya kukutana naye na kumfahamu zaidi," alisema Kikwete.

Kikwete alisema alifurahi zaidi kufanya kazi na Mandela alipoteuliwa kuwa msuluhishi na mpatanishi wa mgororo wa Burundi, nafasi aliyopewa baada ya kifo cha Hayati Julius Nyerere.

Naye Makamu Mkuu wa UDSM, Profesa Willium Anangisye, alisema wakati wa kupigania uhuru wa Afrika Kusini, UDSM ilishiriki kwa kutoa elimu kwa wapigania uhuru wengi.

Alisema pia iliendesha makongamano ya kielimu yaliyolenga kupatikana kwa uhuru wa nchi mbalimbali za Afrika ikiwamo Afrika Kusini.

Mkuu wa Ofisi ya Mratibu Mkazi wa Umoja wa Mataifa na Mpangaji Mkakati, Shabnam Mallick, alisema mchango wa Nelson Mandela katika nchi za Afrika ulijieleza katika upatikanaji wa haki, usawa kwa watu wote.

Alisema UN inatambua mchango wa Nelson Mandela kwa kuadhimisha Siku ya Kimataifa ya Nelson Mandela kila ifikapo Julai 18 kwa kuhamasisha watu kujitolea kwa jamii.

Balozi wa Afrika Kusini nchini Tanzania, Noluthando Mayende-Malepe, alisema katika kumuenzi Nelson Mandela, UN na Balozi wa Afrika Kusini walitoa msaada kwa watoto wanaougua ugonjwa wa saratani katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH).

Alisema walifanya hivyo kwa sababu watoto walikuwa na nafasi maalum katika moyo wa Nelson Mandela ambaye wakati wa uhai wake alikuwa anatenga siku ya kwenda kuwatembelea na kuwapatia misaada.

# Askofu anasa frateli feki kanisani

**Na Vitus Audax,**
MWANZA

ASKOFU Mkuu wa Jimbo Kuu Katoliki la Mwanza, Renatus Nkwande, amemkamata kijana aliyejifanya frateli kwa kuvaa mavazi ya hadhi hiyo na kushiriki shughuli mbalimbali za mafrateri kanisani.

Kijana huyo aliyetajwa kwa jina la Emmanuel Chombo, anadaiwa alikuwa anaogopesha watawa wa Parokia ya Mahandu waliokuliwa wakidai alitaka kuwadhuru, hivyo kutoa taarifa kwa Askofu Mkuu wa Jimbo hilo.

Akithibitisha kumkamata kijana huyo, Askofu Mkuu Nkwande, alibainisha kumtambua, akimtaja kwamba awali alikuwa Bunda mkoani Mara na kanisa liliamua kumchukua na kumsomesha kwa miaka mitatu akiwa na umri mdogo kisha kuhamishiwa Murutunguru.

Alisema kuwa kijana huyo hakusoma seminari kama zilivyo taratibu za kufikia ngazi hiyo ya utumishi kanisani.

"Alikuja Bunda akihitaji msaada wa kusomeshwa. Tukakaa naye Bunda. Baada ya muda tukampeleka Murutunguru Sekondari ambako aliendelea na masomo yake ya kawaida. Hakuwa na nidhamu masomoni na (hivyo) kushindwa kufanya vizuri masomoni," alieleza Askofu Nkwande.

Baada ya kuwa na maendeleo yasiyoridhisha masomoni, kiongozi huyo wa kiroho, alibainisua kuwa waliokuwa wanamlipia ada walisitisha huduma hiyo (kumlipia ada), akatolewa masomoni.

**NAMNA ALIVYONASWA**

Askofu Nkwande, akieleza namna alivyomgundua kijana huyo, alibainisha kwamba, hivi karibuni wakiwa katika maadhimisho ya misa ya upadirisho katika Parokia ya Nyegezi jijini Mwanza, alimwona kijana huyo.

Hata hivyo, Askofu Nkwande alieleza kuwa alipokuwa anafuatilia kujua undani wa kilichokuwa kinajiri, kijana huyo alitoweka. Katika udadisi wake kwa mafrateri waliokuwa naye, mrejesho ni kwamba hawamfahamu.

"Sasa leo (juzi) baada ya kumaliza misa, nikamwona akiwa amejipanga na mafrateli wengine na mavazi katika mstari wa chakula. Nikamwulizi 'wewe ni fratlri wa wapi?'. Akatoa majibu yenye shaka. Ndipo nikafuatilia katika maeneo aliyoyataja ikaonekana ni mwongo, si frateli," Askofu Nkwande alifafanua.

Aliendelea kueleza kuwa baada ya mahojiano zaidi, kijana huyo alikiri kuwa si frateli huku akiomba msamaha. Akamsamehe na kumwonya kuwa "kwa tabia hizo za udanganyifu hawezi kuwa katika utumishi".

"Hatujakaa na kupanga namna ya kufanya juu ya kijana huyu lakini kutokana na tabia zake, hawezi kuendelea katika utumishi kwani anaweza kudanganya hata mahala pengine. Kama kanisa, hatutochoka kumsaidia kwa malezi na makuzi mazuri," alisema.

**UTETEZI WAKE**

Akizungumza baada ya kukamatwa, Chombo alisema ametumikia kama frateri katika Parokia ya Mahandu kwa kipindi kisichozidi mwezi mmoja, huku akimwomba askofu huyo kumsaidia kupata nafasi hiyo.

"Nimekuaibisha sana baba askofu, Ninaomba unisamehe. Lakini ninapenda kuwa na maisha kama haya. Muda mwingine ninashindwa hata kulala ili niwe katika nafasi hii," alidai kijana huyo.




# Kasi maambukizi Ukimwi yamshtua Mpango

**Na Elizabeth John,**
NJOMBE

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, ameshtushwa na kasi ya maambukizi ya virusi vya Ukimwi (VVU) na unyonyeshaji duni mkoani Njombe.

Dk. Mpango aliyasema hayo aliposimama kusalimia wananchi wa Halmashauri ya Mji Makambako akiwa njiani kwenda kwenye ziara ya kikazi mkoani Ruvuma.

"Salamu nyingine naomba niwakumbushe ndugu zangu wa Makambako, Ukimwi bado upo... Tunataka watu waishi muda mrefu, wawe na afya njema ya kujenga nchi yao. Lakini kama ndiyo tunahangaika na magonjwa haya ambayo tunaweza kuepuka, hili si sawa na mimi siwezi kunyamaza.

"Sasa huu ni mji mkubwa wa biashara tena umekaa pazuri. Barabara hiyo inakwenda Mbeya hiyo inakwenda huku na huko. Ukimwi bado upo kwa hiyo nawaomba sana tujitahidi kudhibiti maambukizi mapya. Sasa hivi wastani wa kuishi kwa maisha ya Mtanzania ni miaka 65 tu. Miaka 65 mtu bado ana afya kweli kweli lakini Ukimwi tutapukutika tena tulikuwa tunaenda vizuri lakini tumerudi nyuma kwa hiyo tuzingatie maelekezo ya viongozi wetu wa dini," alisema.

"Ndugu zangu tuzingatie ule ugonjwa unatesa sana. Hata ulichochuma kinaangamia kabisa sasa huu uzembe wa kuanguka ovyo ovyo hapana, kwa hiyo tujikinge," alisisitiza Dk. Mpango.

Kuhusu lishe, Dk. Mpango alisema kulinganisha na takwimu za ubora, mkoa Njombe haufanani na chakula kingi kinachozalishwa katika taifa na mkoa.

"Maana yake ni kwamba tunakula kujaza tumbo. Niwaombe suala la ubora wa lishe ni jambo la msingi sana labda ngoja niliekeze kidogo zipo tafiti za kitaalamu ambazo zinaonyesha ukimchukua mtoto ambaye ana umri wa miaka mitano, ukachukua watoto wawili mmoja alikua na lishe nzuri maana amepata protini, amepata chakula cha wanga, amepata matunda, nyama, mayai, maharage na ndizi na ukichukua watoto wawili mmoja amepata chakula cha kutosha na mwengine hakupata, kwanza hata ukubwa wa ubongo unatofautiana kwa mbali.

"Yule ambaye hakupata lishe bora unakuta kaubongo ni kadogo sana. Uwezo wake wa kufikiri huyu mtoto ni mdogo sana kwa hiyo unakuta sisi ambao tumekaa shuleni kufundisha unaweza kuwa unampiga mtoto mbona haelewi lakini kumbe tatizo alipata lishe ndogo kuanzia alipokuwa tumboni mwa mama yake mpaka alipokuwa anafikisha miaka miwili ya baada kuzaliwa.

"Kwa hiyo ukimpeleka kwenye biashara hawezi, ukimpeleka kwenye michezo ndio kabisa, ukimpeleka kwenye uongozi hawezi. Yaani hakuna mahali anafanya vizuri. Mungu ametujalia chakula tunazalisha kwa wingi lakini tuwahimize wananchi wetu kula chakula ambacho kina virutubisho vya kutosha la sivyo tutaendelea kuzaa watoto wanaonekana wazuri lakini uwezo wao katika mambo mengi kwenye maisha unakuwa mdogo sana," alisema.

Ili kuhakikisha watoto wanakuwa na afya bora, aliwataka wananchi wa Makambako kuhakikisha kuzingatia siku 1,000 za unyonyeshaji. Alisema katika kufanya hivyo, mama baada ya kujifungua na mtoto wake wale chakula chenye virutubisho.

Dk. Mpango pia alizungumzia kilimo cha parachichi na kuwataka wakulima kuacha kuuza matunda ambayo hayajakomaa kwa sababu yanaharibu soko la nje huku akiweka bayana kwamba katika mkoa wa Njombe bado kuna tatizo la kuuza mazao kwa kipimo kilichozidi, maarufu kama lumbesa.

"Sheria ipo nadhani ni ya mwaka 2002 tuzingatie wakulima wetu wanapunjika. Kwa hiyo mshirikiane na Wizara ya Viwanda na Biashara tutumie vipimo sahihi tunapouza mazao ya wakulima wetu. Wananchi hawa wanafanya juhudi kubwa mno kwa hiyo lazima tuwalinde wapate haki ya jasho lao na kwa hili nitaendelea kupiga kelele," alisema.


**icap** Global Health

7th Floor, Jangid Plaza, Plot No. G6, Chaburuma Road (Off-Ali Hassan Mwinyi Road)
P.O. Box 80214, Dar es Salaam, Tel +255 22 2126729/30. Fax +255 22 2121695: Email: icap-tz-info@columbia.edu

## TAARIFA MUHIMU KWA UMMA

ICAP ni Shirika lisilo la Kiserikali linalohusiana na Shule ya Afya ya Umma ya Chuo Kikuu cha Columbia (MSPH) lililosajiliwa Tanzania kama MSPH Tanzania LLC tangu Februari 2005 (SO No.12987). Kwa masikitiko tumepokea taarifa kwamba kuna baadhi ya watu wenye nia ovu ambao wanajitambulisha kuwa wao wanafanya kazi kwa niaba ya ICAP kuajiri wafanyakazi. ICAP inapenda kuuarifu umma wa Watanzania kwamba:

- ICAP haijakasimu kwa taasisi au mtu yeyote mchakato wake wa ajira na tunalaani vikali vitendo vya udanganyifu vinavyofanywa na watu wenye nia ya kujipatia fedha kwa njia za udanganyifu.
- ICAP haina utaratibu wa kudai fedha kwa waombaji wa nafasi za ajira kama sehemu ya mchakato wa ajira kwa mfano wakati wa kuwasilisha maombi au wakati wa usaili.
- ICAP haitahusika na udanganyifu, wizi au hasara yoyote ile ambayo inaweza kusababishwa na mtu yeyote anayeshiriki katika shughuli za kuajiri kwa njia ya udanganyifu.
- ICAP haina utaratibu wa kupokea maombi ya ajira kwa njia ya simu au barua pepe, isipokuwa maombi yote ya ajira hupokelewa kwa njia ya mtandao wa kielektroniki wa ajira kwenye anuani ifuatayo:
  **https://icapacity.icap.columbia.edu/en-us/listing/**
- Maafisa rasilimali watu wa ICAP watatambulika kwa kitambulisho cha wafanyakazi halali na barua pepe ya kazi inayoishia **@cumc.columbia.edu** ambayo hutumiwa kwa mawasiliano yote rasmi. Aidha kikanuni, ICAP haina uvumilivu kabisa kwa mfanyakazi yeyote mwenye tabia za udanganyifu katika kazi.
- Tunawaasa umma wa Watanzania kuwa waangalifu, na ikiwa una maswali yoyote tembelea ofisi kuu ya ICAP Tanzania iliyo Dar es Salaam

BancABC part of atlasmara

# UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

## IMETOLEWA CHINI YA KANUNI YA 7 NA YA 8 YA KANUNI ZA MABENKI NA TAASISI ZA FEDHA (UONESHAJI) YA MWAKA 2014

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30 JUNI 2023
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya /Mwaka wa sasa 30-Jun-23 | Robo Mwaka/Mwaka uliopita 31-Mar-23 |
|---|---|---|---|
| **A** | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 5,985 | 4,270 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 10,506 | 10,417 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 35,787 | 43,973 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 10,484 | 4,775 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 89 | 74 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 98,183 | 98,773 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 128,621 | 127,159 |
| | | - | - |
| 12 | Mali Nyingine | 17,660 | 20,361 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | 1,000 | 1,000 |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 2,070 | 2,286 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **310,386** | **313,089** |
| **B** | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 41,016 | 55,677 |
| 18 | Amana za Wateja | 142,729 | 133,912 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | - | - |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | - | - |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 8 | 0 |
| 27 | Dhima Nyingine | 4,201 | 3,689 |
| 28 | Madeni | 96,250 | 93,051 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **284,205** | **286,329** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI (16 kutoa 29)** | **26,181** | **26,759** |
| **C** | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 139,306 | 139,306 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 1,033 | - |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | (115,460) | (114,427) |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | (1,717) | - 1,138 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 3,018 | 3,018 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **26,181** | **26,759** |
| | | (0) | - |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 6,009 | 1,945 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 9,199 | 8,256 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 6,001 | 6,400 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| **D** | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (I) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 8.43% | 3.63% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 6.83% | 5.49% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 73.27% | 65.49% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 41.44% | 39.65% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 47.21% | 48.36% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | -3.08% | 1.23% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | -0.86% | -2.32% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 JUNI 2023
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya sasa 30-Jun-23 | Robo Mwaka iliyopita 31-Mar-23 |
|---|---|---|---|
| **I** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | (520) | (1,080) |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | - | - |
| | - Hasara Katika Mali | 1,147 | 856 |
| | - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (1,462) | (1,317) |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | (5,844) | (19,359) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | 8,186 | (17) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 512 | (429) |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 2,394 | 514 |
| | - Kodi Iliyolipwa | (59) | (59) |
| | - Mengineyo (bainisha) | - | - |
| | **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **4,355** | **(20,890)** |
| **II** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | - | - |
| | Gawio Lililopokewa | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (630) | (687) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **(630)** | **(687)** |
| **III** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | 3,199 | 242 |
| | Mengineyo (bainisha) | - | 16,352 |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha** | **3,199** | **16,594** |
| | | - | - |
| **IV** | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | - | - |
| | Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | 6,924 | (4,984) |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 118,235 | 123,219 |
| | **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka** | **125,159** | **118,235** |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 30 JUNI 2023
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya Mwaka sasa 30-Jun-23 | Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita 30-Jun-22 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Jun-23 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30-Jun-22 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 10,377 | 10,017 | 20,660 | 20,166 |
| 2 | Gharama za Riba | (4,787) | (4,947) | (9,707) | (9,874) |
| **3** | **Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **5,590** | **5,071** | **10,953** | **10,292** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | 544 | 313 | 553 | 624 |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (300) | - | (300) | - |
| **6** | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | **1,534** | **1,959** | **2,792** | **2,841** |
| 6.1 | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 408 | 248 | 927 | 385 |
| 6.2 | 6.2 Ada na Kamisheni | 377 | 263 | 675 | 552 |
| | 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| 6.3 | 6.4 Mapato Mengine | 749 | 1,448 | 1,190 | 1,904 |
| **7** | **Gharama Zisizo za Riba:** | **(7,887)** | **(7,506)** | **(15,598)** | **(14,492)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (2,865) | (2,613) | (5,560) | (5,160) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | - | - | - | - |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (5,022) | (4,893) | (10,038) | (9,332) |
| **8** | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **(520)** | **(163)** | **(1,599)** | **(735)** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | (59) | - | (117) | (65) |
| **10** | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **(579)** | **(163)** | **(1,717)** | **(800)** |
| 11 | Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha) | - | - | - | - |
| **12** | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **(579)** | **(163)** | **(1,717)** | **(800)** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 172 | 175 | 172 | 175 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | (0.24) | (0.07) | (0.17) | (0) |
| 15 | Mapato yaliyopatikana kwa Kushiriki | - | - | - | - |
| 16 | Idadi ya Matawi | 6 | 6 | 6 | 6 |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | 0 | - | 0 | - |
| (I) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | -0.74% | -0.10% | -1.10% | -0.47% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | -8.74% | -1.25% | -12.97% | -6.14% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 110.72% | 106.77% | 113.48% | 110.35% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 3.19% | 1.36% | 3.12% | 2.77% |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30 JUNI 2023

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **122,954** | **-** | **(114,427)** | **-** | **-** | **3,018** | **11,746** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | (1,717) | - | - | - | **(1,717)** |
| Hisa za upendeleo | 16,352 | | | | | | |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | (1,033) | 1,033 | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **139,306** | **-** | **(117,177)** | **1,033** | **-** | **3,018** | **26,181** |
| | - | - | - | - | - | - | **0** |
| **Mwaka Uliopita** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **122,954** | **-** | **(99,102)** | **2,162.58** | **-** | **989** | **27,004** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | (17,288) | - | - | - | **(17,288)** |
| Hisa za upendeleo | - | - | - | - | - | - | |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | 2,029 | **2,029** |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | 2,163 | (2,163) | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **122,954** | **-** | **(114,427)** | **-** | **-** | **3,018** | **11,746** |

| | Jina | Sahihi | Tarehe |
|---|---|---|---|
| Ofisa Mtendaji Mkuu | I. John | | 21-Jul-23 |
| Mkuu wa Fedha | H. Kharbush | | 21-Jul-23 |
| Mkaguzi Mkuu wa Ndani | J. Kilato | | 21-Jul-23 |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi

| | Jina | Sahihi | Tarehe |
|---|---|---|---|
| 1 Mkurugenzi | P. Ishengoma | | 21-Jul-23 |
| 2 Mkurugenzi | Mr.R. Dave | | 21-Jul-23 |

# Canada yamwaga bil. 330/- elimu, afya

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

CANADA imetoa msaada wa zaidi ya Sh. bilioni 330 (Dola za Canada milioni 178.5) kwa ajili ya miradi ya sekta ya elimu na afya.

Katika fedha hizo, sekta ya elimu kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imepokea Dola za Canada milioni 50 huku sekta ya afya kupitia Wizara ya Afya ikipata Dola za Canada milioni 128.5.

Waziri anayehusika na Maendeleo ya Kimataifa na mwenye dhamana ya Shirika la Maendeleo ya Uchumi nchini humo, Harjit Sajjan, alitangaza msaada huo jana kwenye ziara yake aliyoifanya kwenye wizara hizo jijini hapa.

Sajjan alisema fedha hizo ni kwa ajili ya mradi uitwao 'Kila Binti Asome' utakaotekelezwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF) na mradi wa uwezeshaji kupitia programu za ujuzi utakaotekelezwa na Shirika la Vyuo na Taasisi la Canada. Kila mradi utagharimu Dola za Canada milioni 25.

"Mradi wa Kila Binti Asome unalenga kuboresha upatikanaji wa fursa za elimu na ujuzi kwa mabinti wa Tanzania ili kukuza uwezeshwaji wake na kupata fursa za ajira za staha," alisema.

Pia alisema mradi wa uwezeshaji unalenga kuongeza ushiriki wa kiuchumi kwa wanawake na mabinti wa Tanzania kwa kuimarisha uwezo wa vyuo vya maendeleo 12 na mashirika ya kijamii 16 kutengeneza na kutoa mafunzo ya ujuzi kwa wanawake na mabinti.

"Tunafahamu changamoto za kujifunza na kukuza ujuzi zinazowakabili mabinti wa Tanzania Bara na Zanzibar ikiwamo mzigo wa kazi nyumbani, ukatili wa kijinsia, mila na desturi, ndoa za utotoni," alisema.



Pia alisema elimu kwa wasichana inachukuliwa kwa thamani ndogo na hakuna motisha kwao kumaliza masomo huku akisema shule nyingi hazikidhi mahitaji ya wasichana walio katika kipindi cha balehe.

"Tunapongeza serikali ya Tanzania kwa jitihada zake kwenye kuwezesha upatikanaji wa elimu, Canada imekuwa mshirika wa muda mrefu wa Tanzania katika sekta ya elimu," alisema.

Alisema kuwa kupitia mradi wa kila binti asome utawawezesha waliopo msingi na sekondari haswa kwenye masomo ya sayansi na hisabati.

"Mradi unalenga kuwawezesha mabinti wenye umri wa miaka kati ya 10 hadi 19 kujifunza na kuongeza ujuzi wao ili kuendana na mahitaji ya soko la sasa na ya baadaye nchini Tanzania, pia utatoa fursa za upatikanaji wa njia bora mbadala za kujifunza kwa mabinti wajawazito na waliojifungua ambao wameenguliwa kwenye mifumo rasmi ya elimu," alisema.

Waziri huyo alisema wamedhamiria kusaidia vijana kukuza ujuzi wa kiufundi na mradi huo wa programu ya mafunzo ya ujuzi utatoa usaidizi.

Akizungumzia sekta ya afya, alisema kati ya fedha zilizotolewa Dola za Canada milioni 75 ni kwa ajili ya mfuko wa pamoja wa afya ili kusaidia huduma muhimu za afya za msingi katika kuokoa maisha kama vile utunzaji katika ujauzito na baada ya kuzaa, uzazi wa dharura na utunzaji wa watoto wachanga.

"Fedha hizi ni kwa ajili ya kuhamasisha usawa wa kijinsia kwa wanawake na wasichana katika sekta ya afya, pia tumetoa Dola za Canada milioni 15 kwa ajili ya mradi wa afya na haki za wasichana uliopo Katavi, pia Dola za Canada milioni 15 tumetoa kwa mradi wa kukuza matumaini na maendeleo kwa vijana nchini utatekelezwa mikoa ya Dar es Salaam na Dodoma," alisema.

Pia alisema Dola za Canada milioni 15 zimetolewa ili kuboresha afya kwa wasichana mkoani Tabora huku Dola za Canada milioni 23 kwa ajili ya miradi miwili ya masuala ya chanjo.

### KAULI ZA MAWAZIRI

Waziri wa Elimu, Prof. Adolf Mkenda aliwashukuru Canada kwa msaada huo wa kielimu utakaosaidia kuendelea kuchochea mapinduzi ya elimu Tanzania.

"Msaada huu ni unatokana na Rais kuendelea kujenga mahusiano mazuri ya kidiplomasia, kama nilivyokueleza Waziri sisi Tanzania tunafanya mageuzi makubwa ya elimu kwasasa miaka ya lazima ya mtoto kukaa shuleni ni saba na matokeo yake wanamaliza wakiwa na miaka 13 ambayo hairuhusu kuingia soko la ajira," alisema.

Alisema hatua ya kwanza ya elimu ya lazima kuwa miaka 10 badala ya saba mchakato wake unaendelea na wanasubiri kibali cha mwisho ili kuanza utekelezaji.

Aidha, Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, alisema fedha zilizotolewa kwa sekta ya afya ni zaidi ya Sh. bilioni 240 na kati ya hizo Sh.bilioni 140 zinaingia serikalini kwa ajili ya kuchangia mfuko wa afya wa pamoja.

"Fedha hizi zitatumika kikamilifu kuleta matunda yaliyokusudiwa, fedha hizi zimeshaingia na kwa upande wa serikali tayari tumepokea Sh. bilioni 94 kwa ajili ya mfuko huu na ndani ya siku chache zitapelekwa moja kwa moja kwenye zahanati, vituo vya afya na hospitali za serikali," alisema.


## MINIMUM DISCLOSURES OF BANK CHARGES AND FEES

| | PRICING (TZS) | PRICING (US $ / EUR) | PRICING (GBP) |
|---|---|---|---|
| **PERSONAL BANKING** | | | |
| **SAVINGS ACCOUNT** | | | |
| **IZZE** | | | |
| Account Opening Fee | Free | NA | NA |
| Opening balance | Free | NA | NA |
| Minimum Operating Balance | NIL | NA | NA |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 10,000.00 | NA | NA |
| Monthly Service Fee | Free | NA | NA |
| **FAHARI** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 10,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Minimum Operating Balance | TZS 10,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 50,000.00 | $ 100.00 | £ 100.00 |
| Monthly Service Fee | TZS 1,500.00 | $ 2.00 | £ 2.00 |
| **MWANGAZA JUNIOR ACCOUNT** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 20,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Minimum Operating Balance | TZS 20,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 20,000.00 | $ 500.00 | £ 500.00 |
| Monthly Service Fee (1 free w/drawal per quarter) | Free | Free | Free |
| Extra fee for more than 1 w/drawal per quarter | TZS 5,500.00 | $ 2.00 | £ 2.00 |
| **WEKEZA SAVINGS ACCOUNT (BALANCE BUILD UP)** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | N/A |
| Opening balance | Free | Free | N/A |
| Minimum Operating Balance | NIL | NIL | N/A |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 100,000.00 | $ 25.00 | N/A |
| Monthly Service Fee* | Free | Free | N/A |
| **CURRENT ACCOUNT** | | | |
| **AMANA** | | | |
| Account Opening Fee | Free | N/A | N/A |
| Opening balance | TZS 20,000.00 | N/A | N/A |
| Minimum Operating Balance | TZS 3,000.00 | N/A | N/A |
| Minimum Interest Bearing Balance | N/A | N/A | N/A |
| Monthly Service Fee* | TZS 3,000.00 | N/A | N/A |
| **MARIDHAWA** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 25,000.00 | $ 25.00 | £ 25.00 |
| Minimum Operating Balance | TZS 6,000.00 | $ 5.00 | £ 5.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | NA | NA | N/A |
| Monthly Service Fee* | TZS 10,000.00 | $ 10.00 | £ 10.00 |
| **PREMIUM** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 35,000.00 | $ 30.00 | £ 30.00 |
| Minimum Operating Balance | NIL | NIL | NIL |
| Minimum Interest Bearing Balance | NA | NA | NA |
| Monthly Service Fee* | TZS 15,000.00 | $ 10.00 | £ 10.00 |
| **SME BANKING** | | | |
| **AMANA BIZ ACCOUNTS** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 50,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Minimum Operating Balance | TZS 50,000.00 | $ 100.00 | £ 100.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | NA | NA | NA |
| Monthly Service Fee* | TZS 15,000.00 | $ 15.00 | £ 15.00 |
| **SME TIERED CURRENT ACCOUNT** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | NA |
| Opening balance | TZS 100,000.00 | $ 100.00 | NA |
| Minimum Operating Balance | TZS 1,000,000.00 | $ 1,000.00 | NA |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 5,000,000.00 | $ 5,000.00 | NA |
| Monthly Service Fee* | TZS 20,000.00 | $ 15.00 | NA |
| **JAMII CURRENT ACCOUNT** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | Free | Free | Free |
| Minimum Operating Balance | TZS 100,000.00 | $ 100.00 | £ 100.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 5,000,000.00 | $ 50,000.00 | £ 50,000.00 |
| Monthly Service Fee* | Free | Free | Free |
| **CORPORATE BANKING** | | | |
| **CORPORATE CURRENT ACCOUNTS** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 500,000.00 | $ 250.00 | £ 250.00 |
| Minimum Operating Balance | NIL | NIL | NIL |
| Minimum Interest Bearing Balance | NA | NA | NA |
| Monthly Service Fee* | TZS 25,000.00 | $ 20.00 | £ 15.00 |
| **CORPORATE CALL ACCOUNTS** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 10,000,000.00 | $ 10,000.00 | £ 10,000.00 |
| Minimum Operating Balance | TZS 10,000,000.00 | $ 10,000.00 | £ 10,000.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 1.00 | $ 1.00 | £ 1.00 |
| Monthly Service Fee* | TZS 20,000.00 | $ 20.00 | £ 15.00 |
| **CORPORATE TIERED INTEREST ACCOUNTS** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | NA |
| Opening balance | TZS 500,000.00 | $ 250.00 | NA |
| Minimum Operating Balance | NIL | NIL | NA |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 50,000,000.00 | $ 100,000.00 | NA |
| Monthly Service Fee* | TZS 25,000.00 | $ 20.00 | NA |
| **GENERAL CHARGES** | | | |
| Bankers Cheque | TZS 50,000.00 | $ 25.00 | N/A |
| DISHONORED/UNPAID CHEQUE | | | |
| Fund related | TZS 120,000.00 | $ 50.00 | N/A |
| Technical | TZS 30,000.00 | $ 50.00 | N/A |
| **Cheque book Processing Fee:** | | | |
| 25 leaves | TZS 15,000.00 | $ 15.00 | £ 15.00 |
| 50 leaves | TZS 25,000.00 | $ 20.00 | £ 20.00 |
| 100 leaves | TZS 50,000.00 | $ 35.00 | £ 35.00 |
| Uncollected cheque book after 3 months | TZS 15,000.00 | $ 15.00 | £ 15.00 |
| 3rd party encashment (with 3rd party indemnity) | TZS 25,000.00 | 1% Per Cheque + $20 | 1% Per Cheque +$20 |
| Stop Payment Charges | TZS 30,000.00 | $ 25.00 | £ 25.00 |
| **TRANSACTIONAL SERVICE FEES** | | | |
| **With banks via Standing Orders** | | | |
| Standing Order - internal same customer ( set up fee - once off) | Free | Free | Free |
| Standing Order - internal other customers ( per transaction) | Free | Free | Free |
| Standing Order - Other local bank | TZS 20,000.00 | $ 10.00 | £ 10.00 |
| Amendment | Free | Free | Free |
| **DEPOSIT/WITHDRAWAL TRANSACTIONS:** | | | |
| Cash Deposit at Branch | Free | Free | Free |
| Cash Deposit at Branch coins above 100,000 | 5% Min 10,000 | NA | NA |
| Cash Deposit at Branch small denominations less than 50USD (USD 1,2,5,10,20) equal and above USD 500 | NA | 3% of FCY currency value | 3% of FCY currency value |
| With Account Transfers (Internal) | Free | Free | Free |
| Cheque deposit | Free | Free | Free |
| Cash withdrawal Personal Banking ( over the counter) up to 2m | TZS 3,500.00 | 1% Min 5 | 1% min 5 |
| Cash withdrawal Personal Banking ( over the counter) btn 2m to 20m | TZS 4,000.00 | 1% Min 5 | 1% min 5 |
| Cash withdrawal Personal Banking ( over the counter) above 20m | 0.15% Max 50,000 | 1% Min 5 | 1% min 5 |
| Cash withdrawal SME ( over the counter) | 0.15%Min 3,000 Max 20,000 | 1% Min 5 | 1% min 5 |
| Cash withdrawal Corporate Banking | 0.15%Min 3,000 Max 100,000 | 1% Min 5 | 1% min 5 |
| Deposit charges - Financial Institution. | Free | Free | Free |
| Deposit charges - Financial Institution - small denominations | Free | 3%On small denominations above $500 | 3%On small denominations above $500 |
| Account Closure | TZS 10,000.00 | $ 10.00 | £ 10.00 |
| Dormant Account Reactivation | NIL | NIL | NIL |
| Dormant Account monthly fee | NIL | NIL | NIL |
| Premature/cancellation fixed deposit fee | 50% Accrued Interest is Forfeited. Breaking 1st month all interest forfeited | 50% Accrued Interest is Forfeited. Breaking 1st month all interest forfeited | 50% Accrued Interest is Forfeited. Breaking 1st month all interest forfeited |
| Monthly statements | Free | Free | Free |
| Interim Statements (per page) | TZS 2,000.00 | $ 1.00 | £ 1.00 |
| Search fee documents (after 3 months) | TZS 80,000.00 | $ 40.00 | £ 40.00 |
| Audit confirmation | TZS 75,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Balance Certificate | TZS 50,000.00 | $ 30.00 | £ 30.00 |
| Reference Letter | TZS 50,000.00 | $ 30.00 | £ 30.00 |
| Inter Account Transfers | Free | Free | Free |
| T T Outward local - TISS | TZS 11,800.00 | $ 10.00 | N/A |
| T T Outward local - EFT | TZS 3,000.00 | N/A | N/A |
| T T Inward local TISS | Free | Free | N/A |
| Salary processing (per entry) | TZS 1,500.00 | $ 1.00 | £ 1.00 |
| International Outward T T | N/A | $50 + Other overseas bank chrges | $50 + Other overseas bank chrges |
| International Inward T T | N/A | Free | Free |
| Travellers Chq. Deposit | N/A | N/A | N/A |
| Foreign BankDrafts | N/A | $ 50.00 | £ 30.00 |
| Outward Cheque for Collection | N/A | N/A | N/A |
| Outward Bills for collection | N/A | 0.25% min 50 + $ 50 (courier charge) | 0.25% min 50 + $ 50 (courier charge) |
| Inward Bills for Collection | N/A | 0.25% MIN 50 | 0.25% MIN 50 |
| Advising fee (Inward Bill & LCs ) | N/A | $ 200.00 | £ 200.00 |
| Travellers Chq. (Issue) | N/A | N/A | N/A |
| Letters of Credit | N/A | 1% per qtr + $ 50 (total min $250) | 1% per qtr + $ 50 (total min $250) |
| Bank Guarantees | 1% Per Qtr Min $ 200 | 1% Per Qtr Min $ 200 | 1% Per Qtr Min $ 200 |

| AGENCY BANKING FEE | |
|---|---|
| Deposit | Free |
| Bill payment | Free |

**Withdrawal Fees**

| Transaction tiers | BancABC Fees | Government Levy | Total Fees |
|---|---|---|---|
| 0-999 | N/A | - | N/A |
| 1,000-1,999 | 300 | 10 | 310 |
| 2,000-2,999 | 300 | 11 | 311 |
| 3,000-3,999 | 300 | 19 | 319 |
| 4,000-4,999 | 300 | 39 | 339 |
| 5,000-6,999 | 500 | 70 | 570 |
| 7,000-9,999 | 500 | 88 | 588 |
| 10,000-14,999 | 600 | 224 | 824 |
| 15,000-19,999 | 600 | 427 | 1,027 |
| 20,000-29,999 | 600 | 672 | 1,272 |
| 30,000-39,999 | 700 | 770 | 1,470 |
| 40,000-49,999 | 800 | 1,050 | 1,850 |
| 50,000-99,999 | 900 | 1,435 | 2,335 |
| 100,000-199,999 | 1,000 | 1,771 | 2,771 |
| 200,000-299,999 | 1,100 | 2,058 | 3,158 |
| 300,000-399,999 | 1,200 | 2,450 | 3,650 |
| 400,000-499,999 | 1,200 | 2,870 | 4,070 |
| 500,000-599,999 | 2,000 | 3,640 | 5,640 |
| 600,000-699,999 | 2,000 | 4,480 | 6,480 |
| 700,000-799,999 | 2,000 | 4,970 | 6,970 |
| 800,000-899,999 | 2,000 | 5,264 | 7,264 |
| 900,000-1,000,000 | 2,000 | 6,230 | 8,230 |
| 1,000,001-2,000,000 | 2,300 | 6,580 | 8,880 |
| 2,000,001-3,000,000 | 2,500 | 6,580 | 9,080 |
| 3,000,001 na zaidi | N/A | 7,000 | N/A |

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tahadhari kubwa inatakiwa kukabiliana na mvua El- Nino

**MAMLAKA** ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) juzi ilitoa tahadhari ya kuwapo kwa mvua ya El- Nino katika kipindi cha msimu wa vuli kuanzia Oktoba hadi Desemba mwaka huu. Kwa mujibu wa mamlaka hiyo, tahadhari hiyo imetokana na kujiridhisha kupitia mifumo yake na kwamba uwezekano wa kuwapo kwa mvua hiyo ni asilimia 90.

Taarifa ya mamlaka hiyo ilitaja mikoa ambayo inaweza kukumbwa na mvua hiyo kuwa ni ya Nyanda za Juu Kaskazini ambayo ni Arusha, Tanga, Kilimanjaro na Manyara, na ile ya ukanda wa pwani ambayo ni Dar es Salaam, Pwani, Zanzibar, Lindi na Mtwara.

Aidha, kutokana na kuwapo kwa tishio la mvua hiyo, TMA ilisema inaendelea kufuatilia mwenendo huo na kutoa taarifa za mara kwa mara na kuuhabarisha umma juu ya uwezekano wa kuwapo au kupungua kwa tishio la mvua hiyo ambayo ni tishio kwa masuala ya uchumi na kijamii.

Kwa ujumla, taarifa ya TMA kuhusu kuwapo kwa mvua hiyo imetolewa katika kipindi kizuri, si chini ya miezi mitatu, tangu kuwapo kwa utabiri huo hali ambayo itasaidia mamlaka mbalimbali zikiwamo zile zinazojihusisha na miundombinu, kilimo na ufugaji na uvuvi, kuchukua tahadhari katika kukabiliana na majanga yanayoweza kujitokeza. Pia taarifa hiyo inatoa fursa kwa taasisi mbalimbali kama vile idara za maafa ngazi ya wilaya hadi taifa kujizatiti katika kukabiliana na majanga yoyote yatakayosababishwa na mvua hiyo.

Pamoja na kwamba mvua za El-Nino zilishawahi kutokea nchini mwaka 1997/98, watu waliokuwapo wakati huo wana kumbukumbu rasmi juu ya kilichotokea, hivyo ni rahisi kuwaelimisha wale wa kizazi kipya- ambao walikuwa hawajazaliwa wakati huo kuhusu namna ya kuchukua tahadhari.

Katika kipindi hicho, shughuli mbalimbali zikiwamo za uzalishaji na uchukuzi kwa maana ya usafirishaji wa abiria na mizigo zilikwama. Baadhi ya barabara na madaraja vilibomoka, hivyo kusababisha rasilimali fedha nyingi kutumika katika ukarabati na matengenezo ya miundombinu ya muda.


Mkoani Dar es Salaam, mathalan, baadhi ya madaraja yakiwamo ya Mlalakuwa na Segerea yalisombwa na mvua hizo na mawasiliano kati ya Morogoro na Iringa yalikatika baada ya madaraja katika eneo la Iyovi kuvunjika. Hatua hiyo ilisababisha Jeshi la Ulinzi la Wananchi Tanzania (JWTZ) Kikosi cha Ujenzi Ngerengere kufanya kazi ya ziada ya kutengeneza madaraja ya muda. Maafa zaidi yaliyopatikana ni watu kupoteza maisha kutooana na nyumba kubomoka wakati wamelala na ajali zilizosababisha magari kusombwa na maji ya mvua yakiwa barabarani.

Wahenga wanasema kinga ni bora kuliko tiba. Kwa mantiki hiyo, tahadhari zinapaswa kuchukuliwa mapema katika ngazi zote husuan katika mikoa iliyotajwa kuwa inaweza kukumbwa na mvua hizo.

Jambo la kwanza linalopaswa kufanyika ni elimu kwa wananchi kuhusu kuchukua tahadhari dhidi ya mvua hizo. Kwa wale wanaoishi mabondeni au kwenye maeneo ya mikondo mikubwa ya maji majira ya mvua wanatakiwa kupewa muda wa kuyahama maeneo hayo kabla ya kukutwa na majanga.

Idara ya Maafa iliyo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu ambayo jukumu lake kuu ni kupambana na majanga mbalimbali, kutokana na tahadhari hiyo, inatakiwa kuanza kufanya maandalizi dhidi ya athari mbalimbali zinazoweza kujitokeza, kubwa ni kuchukua tahadhari ili kuzuia madhara kuwa makubwa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Mgambo ya nini mateso haya kwa wamachinga

Na Beatrice Shayo

**KUNA** haja ya serikali kuangalia upya mgambo wa jiji na miji na kusaidia kujibu maswali watu wanayojiuliza wamewekwa kwa ajili ya kuharibu bidhaa za wamachinga au pengine hawajui majukumu yao?

Kuna malalamiko kuwa huenda hawajui majukumu yao ya kazi, ni vizuri wakaanza kuelimishwa ndipo waingie mitaani badala ya kutekeleza majukumu na kulalamikiwa kuwa ni kinyume cha utaratibu.

Mgambo hao, jambo la kwanza wanadaiwa kukiuka haki za binadamu na kuharibu bidhaa za wamachinga kinyume cha utaratibu, ndiyo maana napata wasiwasi huenda hawayajui majukumu yao.

Ipo haja ya serikali kuangalia namna ya kufanya maboresho kuhusu mgambo au kuwaondoa kuliko kuendelea kuwatesa baadhi ya watu wakiwa katika biashara ambazo wanatumia pesa, muda na juhudi kuzifanikisha ili kumudu maisha yao.

Hivi karibuni nimeshuhudia tukio nikiwa Mtaa wa Msimbazi Kariakoo jijini Dar es Salaam, nilipokutana na mgambo wenye sare za suruali nyeusi na fulana nyekundu. Nilichogundua ni kwamba kamatakamata yao wanaweza hata kuondoka na mkono wa mmachinga.

Nalazimika kusema wanafanyakazi kinyume cha sheria nikiomba serikali ikaangalia upya mienendo hii. Nilijiuliza maswali mengi hivi kazi yao ni kuwatesa hao wamachinga ambao wamepanga bidhaa maeneo yasiyoruhusiwa au walitakiwa kuwachukulia hatua nyingine?

Wanamgambo hao ambao walikuwa wameshikilia fimbo ya chuma wakikatisha mitaa ya Msimbazi, wanavyoonekana ni kama askari wanaokwenda vitani wanaotumia nguvu iliyopitiliza.

Nilishuhudia mmachinga aliyekuwa ameweka bidhaa katika sanduku la mbao, mgambo alimnyang'anya na kulivunjavunja, aliona kama haitoshi vinywaji alivyokuwa navyo akavipondaponda na kuvitoboa na fimbo ya chuma baadhi vikapasuka. Wapita njia walioshuhudia walijiuliza kwa nini wanamgambo hawa wanafanya hivi? Walikuwa wanaongea huku wakitembea wakisema kuwa wanachokifanya sio sawa mmoja wa wanamgambo alisikia malalamiko na kwenda kumkataza asiendelee kupasua vinywaji vya mfanyabiashara huyo.

Mgambo yule alimsikiliza na kuacha lakini alimtolea lugha ya vitisho akifoka 'nitakupasua'.

Awali, wakati kijana yule anapinga kupasua chupa za maji na soda alimjia juu na kumkunja mithili ya kutaka kupigana naye.

Tukio hilo liliwahuzunisha baadhi ya wapita njia na kumwonea huruma kijana yule kwa kitendo alichokifanyiwa.

Wanamgambo hao walimuacha kijana yule huku akipanga upya bidhaa zake ambazo hazikupasuka katika tenga alilokuwa amehifadhia vinywaji hivyo.

Nilibaki na maswali hawa mgambo kulikuwa na haja gani ya kuharibu hizo bidhaa? Nguvu kubwa wanayoitumia ni nani anayewapa jeuri hiyo? Kijana huyo kama ana makosa kwa nini hajapelekwa sehemu akawajibishwe kwa mujibu wa sheria zilizowekwa na siyo kuharibu mali zake?

Kazi ya mgambo ni kuharibu bidhaa za watu na kwenda kufanya uharibufu? Kwani nini wanawaharibia bidhaa na hata kuwapiga? Kulikuwa na haja gani ya kuharibu vinywa kama hawakuwa tayari kumchukulia hatua? Ni kwa vipi unapasua vinywaji vyake na kutimka?

Hoja yangu sio kwamba nataka kumtetea huyo kijana kufanya biashara katika hayo maeneo yaliyokatazwa hapana. Kilichonikwaza ni uharibifu wanaoufanya hao askari mgambo na kuwaongezea watu maumivu na umaskini kuliko kuwaonya na kuwachukulia hatua zisizowaletea hasara ya mali.

Askari hao baada ya kupiga hatua tano wakaanza kusema tunamsaka yule anayetuzungumzia vibaya katika hiki kijiwe leo hajafika tutamrudia tena mpaka tumpate.

Unaweza kusema wanachokifanya huko mitaani ni kuwaonea watu na kuwatisha badala ya kusimamia kazi waliyopewa kwa uadilifu kama huyo mmachinga amekosea akamatwe na kufikishwa katika vyombo vya maamuzi badala ya kumfanyia vitendo vya uonevu.

Nashauri hao mgambo kama hawawezi kutekeleza majukumu yao kwa weledi ni bora wakaondolewa malalamiko ni mengi dhidi yao.



Naibu Waziri Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Jumanne Sagini (kushoto), akizungumza baada ya kukagua ujenzi wa jengo la polisi Wilaya ya Butiama ambapo limepatiwa kiasi cha Sh. milioni 800, Sh. milioni 500 tayari zimeshatolewa kuendelea na shughuli za ujenzi. **PICHA: WMN**

# Kesi kocha wa Simba yakwama tena

**Na Kulwa Mzee**

UPELELEZI wa kesi ya kusafisha kilogramu 34.89 za dawa za kulevya aina ya heroin, inayomkabili aliyekuwa Kocha wa Makipa wa Klabu ya Simba, Muharami Seltani na wenzake, haujakamilika. Upande wa Jamhuri unasubiri vielelezo kutoka taasisi ya masuala ya mtandao.

Shauri hilo lilikuja kwa ajili ya kutajwa jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Mary Mario.

Akiiwakilisha Jamhuri, Wakili wa Serikali, Erick Kamala alidai upelelezi wa kesi hiyo haujakamilika. Wanasubiri vielelezo kutoka taasisi ya masuala ya mtandao, hivyo akaomba mahakama ipange tarehe nyingine ya kutajwa.

Maombi ya wakili yalikubaliwa. Kesi iliahirishwa hadi Agosti 2, mwaka huu.

Washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni mmiliki wa Kituo cha Cambiasso Sports Academy kilichoko Tuangoma, Manispaa ya Kigamboni.

Wengine ni: Maulid Zungu, maarufu Mbonde; Said Abeid, fundi selemala; John Andrew maarufu Chipanda, mfanyakazi wa Kituo cha Cambiasso; na Sara Joseph.

Washtakiwa hao wanadaiwa kuwa Oktoba 27, 2022, huko Kivule, jijini Dar es Salaam, walikutwa wakisafirisha dawa za kulevya aina ya heroin kilogramu 27.1.

Katika shtaka la pili, inadaiwa kwamba, Novemba 4, 2022, eneo la Kamegele wilayani Mkuranga, mkoani Pwani kwa pamoja walikutwa wakisafirisha kilogramu 7.79 za dawa za kulevya aina ya heroin.

# TAWA yabaini mbinu tatu mpya majangili wa tembo

**Na Joseph Mwendapole**

MAMLAKA ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA) imebaini mbinu tatu mpya zinazotumiwa na majangili wa tembo kukwepa kukamatwa, ikiwamo kuyawekea kemikali meno ya wanyamapori hao ili yasionekane katika mifumo ya ukaguzi kwenye viwanja vya ndege.

Imetaja mbinu nyingine ni baadhi ya majangili kuyasaga meno hayo na kuyasafirisha kama poda, hali ambayo inawafanya wakaguzi kushindwa kubaini imetokana na meno ya tembo.

Jana, Ofisa Wanyamapori Daraja la I (TAWA), Tryphone Kanon, alibainisha hayo katika semina kwa wahariri wa vyombo habari mjini Bagamoyo.

Semina hiyo ya siku mbili imeratibiwa na Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira (JET) kupitia mradi wa Tuhifadhi Maliasili unaofadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Marekani (USAID).

Alitaja mbinu ya tatu mpya kuwa ni kuyaongezea thamani meno ya tembo kwa kutengeneza bidhaa na kuziwekea mapambo na urembo wa aina mbalimbali ili kuwahadaa wakaguzi katika viwanja vya ndege.

Alisema mamlaka za serikali zimekuwa zikijitahidi kuongeza ulinzi katika maeneo ya bandarini na viwanja vya ndege kadri majangili hao wanapokuja na mbinu mpya.

"Hawa watu wamekuwa wakibadili mbinu mara kwa mara kukwepa kukamatwa. Na sisi tunajiimarisha kiintelijensia kila siku, tuna panya wa Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA), tuna mbwa wanaotusaidia katika ukaguzi na wengi wamekuwa wakikamatwa wakijaribu kuvusha meno hayo.

"Hivi karibuni alikamatwa raia wa China, akiwa ameyatengenezea bidhaa za urembo mbalimbali. Kwa kawaida jino la tembo likipita katika mashine ya ukaguzi, linaonekana kwamba hii ni jino la tembo.

"Kwa hiyo, walipoona wanakamatwa wakaanza kuzisaga na kujaza ile poda kwenye chupa ya chai. Kwa hiyo, si rahisi kwa mashine kubaini kwamba ni jino la tembo," alisema.

Ofisa huyo wa TAWA alisema kwa miaka hivi karibuni wamejitahidi kukabiliana na ujangili wa tembo mpaka kufikia hatua ya kukomesha kabisa mauaji ya tembo tofauti na miaka ya nyuma ambapo tembo 50 walikuwa wakiuawa na majangili kwa mwaka.

Alisema ujangili wa tembo umekuwa ukihusisha mtandao mpana unaoanzia ujangili wa daraja la kwanza mpaka daraja la tano, daraja la kwanza likihusisha watu wanaoishi pembezoni mwa hifadhi ambao wanalijua pori au hifadhi vizuri.

Kanon alisema watu hao ndio huwaongoza majangili kujua mahali tembo waliko wakati wa kiangazi na wakati wa jua kwani siyo rahisi kwa mtu mgeni kufahamu tabia za kuhamahama za wanyama hao.

"Daraja la pili ni wale majangili wanaoua tembo na katika daraja hilo la pili, kuna wale tunaowaita dakika sita ambao wana uwezo mkubwa wa kukata jino la tembo haraka ndani ya muda mfupi sana," alisema.

Aliongeza kuwa majangili daraja la tatu ni madalali ambao wanawawezesha wauaji wa tembo katika maeneo yaliyohifadhiwa na kisha kuyakusanya na kuyasafirisha kwenda maeneo ya mijini tayari kwa biashara.

"Majangili daraja la nne ni wale wanaokusanya meno hayo na kuyasafirisha nje ya nchi wakati majangili daraja la tano ni wale majangili wakubwa ambao wengi wako nje ya nchi na mfano mzuri wa watu wa aina hiyo ni yule malkia wa pembe za ndovu ambaye alifungwa," alisema.

Kanon alitaja mbinu walizotumia kutokomeza mtandao huo kuwa ni kufuata mnyororo wa watu wote wanaonufaika na biashara ya pembe za ndovu na kuwafikisha mahakamani ushahidi unapopatikana.

Alisema majangili hao wamekuwa wakitumia mbinu mbalimbali kuwaua tembo hao ikiwamo matumizi ya sumu kwenye maboga, mitego ya aina mbalimbali na sehemu kubwa ya mauaji ya tembo hufanywa kwa kutumia silaha za moto.

TANGAZO MAALUM
KIWANJA KINAUZWA
KAOLE-BAGAMOYO


BEACH PLOT
KIWANJA KINAMILIKIWA KIHALALI
AREA:1.238HA ≈ 3.059 ACRES ≈ 12,380 SQUARE METERS
TITTLE NO: 11422PWN
L.O.NO. 179016
L.D.NO. BAG/6514
TAREHE YA USAJILI: 06.08.2022
TERM: 33 YEARS
KWA MAWASILIANO PIGA SIMU:
0713646776 / 0718 799957
0713 939377



Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara, Hashil Abdallah (katikati), akikata utepe ikiwa ni ishara ya uzinduzi wa magari ya biashara aina ya Ashok Leyland yanayotengenezwa nchini India kwa ajili ya soko la Tanzania. Wa pili kulia ni Balozi wa India nchini, Binaya Pradhan na viongozi wengine waliohudhuria hafla hiyo jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: SABATO KASIKA**

VITA DHIDI YA AJALI BARABARANI

# Kampuni yafadhili mafunzo kwa polisi

## ●Madereva wazembe, trafiki wala rushwa kukiona

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Superdoll imeguswa na kauli ya Rais Samia Suluhu Hassan dhidi ya ajali za barabarani zinazogharimu maisha ya watu. Imefadhili mafunzo maalum kwa polisi kukabiliana na ajali hizo.

Chini ya Mwenyekiti wake, Seif Ally, kampuni hiyo iliandaa mafunzo maalum ya siku tatu kuanzia Jumatatu ya juma hili katika ukumbi wake jijini Dar es Salaam, kwa wakuu wa usalama barabarani wa mikoa na wakaguzi magari.

Ni mafunzo yaliyoandaliwa kwa lengo la kuwajengea uwezo maofisa hao ili kuendana na mabadiliko ya kiteknolojia katika eneo hilo la usalama barabarani.

Katika mafunzo hayo, kampuni hiyo ilitumia wataalamu wake wabobevu katika ukaguzi wa magari, uchunguzi wa ajali za barabarani na mifumo ya ufuatiliaji mienendo ya madereva wa magari yake - kuwaongeza ujuzi maofisa hao wa Jeshi la Polisi ili kupunguza kwa kiwango kikubwa kama si kumaliza kabisa ajali za barabarani nchini, ambazo Rais Samia hivi karibuni alinyooshea kidole kutoa salamu za rambirambi kutokana na vifo vya ajali hizo nchini.

Kwa mujibu wa Seif, mbali na kutumia wataalamu wake, kampuni hiyo pia imewaleta wataalamu kutoka nje ya nchi kutoa mafunzo kwa maofisa hao wa Jeshi la Polisi.

Katika mafunzo hayo, Kampuni ya Superdoll pia imewashirikisha wataalamu kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Mamlaka ya Udhibiti wa Bima nchini (TIRA), Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Ardhini (LATRA), Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) na baadhi ya vyuo vya mafunzo ya udereva nchini.

Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani, Ramadhani Ng'azi, aliyataja mafunzo hayo ni fursa kwa makamanda wa usalama barabarani na wakaguzi wa magari mkoa kujengeana uwezo ili kuwa na utendaji unaozingatia weledi, tija, nidhamu na uadilifu. "Superdoll wanayo mitambo ya kisasa kabisa ya kusimamia magari yao. Kwa kipindi cha miaka 10, magari yao hayajapata ajali yoyote. Tumeona hapa wanafanyaje kwenye eneo hilo.

"Tumejionea namna Superdoll wanavyodhibiti mwenendo wa madereva na tabia zao, pia mwenendo wa gari linapokuwa barabarani. Pia wanayo programu ya mafunzo kazini kwa madereva wao, utaona ni kampuni ambayo imejitosheleza vizuri," alisifu Kamanda Ng'azi.

Alisema kampuni zingine zinapaswa kuiga utendaji wa Superdoll katika kudhibiti mienendo ya madereva badala ya kuacha jukumu hilo kwa Jeshi la Polisi peke yake.

Jumanne Muliro, Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, wakati wa kufunga mafunzo hayo juzi, aliwataka maofisa waliopewa mafunzo hayo kuhakikisha wanakwenda kutokomeza rushwa na kuimarisha utendaji unaozingatia maadili na weledi katika maeneo yao ya kazi.

Kamanda Muliro alieleza kuchukizwa na vitendo vya baadhi ya askari na maofisa wa jeshi hilo wanaoendekeza rushwa, akisema:

"Ofisa mzuri anatakiwa asisite kufanya uamuzi wa kiutendaji. Mtu akifanya vizuri apongezwe, anayefanya vibaya achukuliwe hatua mara moja, lakini usimwonee mtu.

"Watu waliofanya vibaya katika eneo letu la usalama barabarani hivi karibuni, sikusita kuchukua hatua palepale. Tunapobaini huyu mtu hana sifa za kuwa pale na kuendelea kutuabisha kwa vitendo vya rushwa, tunachukua hatua mara moja."

Baada ya kupewa mafunzo, washiriki 121 wa mafunzo, pamoja na mambo mengine, waliazimia kwenda kushughulika na askari wasio waadilifu wanaoendekeza rushwa toka kwa madereva wazembe.

Pia waliazimia kwenda kuwawajibisha askari wanaowabambika makosa madereva na kuwa na mikakati ya kukabiliana na ajali za barabarani katika maeneo yao ya kazi.

Wakati wa ufunguzi wa mafunzo hayo Jumatatu, Mwenyekiti wa Superdoll, Seif, alisema lengo la kuandaa mafunzo hayo ni kuunga mkono jitihada za serikali katika kukabiliana na ajali za barabarani zinazogharimu maisha ya watu wengi nchini.

Alisema Tanzania ni nchi salama kiulinzi, lakini haiko salama kwa ajali za barabarani, akieleza kuguswa na kauli ya Rais Samia ya kuchoshwa na ajali hizo.

Alisema kuwa licha ya mafunzo hayo kugharimu fedha nyingi, wameona kuna haja kuyatoa kwa maofisa hao wa Jeshi la Polisi ili kukabiliana na ajali nchini.

Seif alisema kuwa ili nchi iwe salama dhidi ya ajali barabarani, kunahitaji kufanyike mambo matatu: Utii wa sheria na kanuni; mafunzo endelevu; na kuwekeza katika teknolojia na ubunifu.

Kwa mujibu wa Kikosi cha Usalama Barabarani, jumla ya watu 886 walipoteza maisha katika kipindi cha kati ya Januari na Novemba mwaka jana (2022) kutokana na ajali za barabarani.

Vilevile, watu 573 walipata majeraha kutokana na ajali 1,422 zilizorekodiwa na kikosi hicho kwa kipindi tajwa. Ni ongezeko la ajali 11 kulinganisha na zilizotokea katika kipindi kama hicho mwaka 2021 zilizosababisha vifo vya watu 1,008 na kujeruhi 1,496.

# Bodaboda washtuka jina la chama chao kutumika vibaya

**Na Halfani Chusi**

CHAMA cha Madereva na Wamiliki wa Pikipiki Mkoa wa Dar es Salaam (CMPD) kimepanga kufungua shauri mahakamani dhidi ya taasisi kutumia jina la chama hicho kama mmoja wa wanachama wake ilhali si kweli.

Kimebainisha kuwa kitalazimika kufungua shauri mahakamani ikiwa kampuni hiyo itashindwa kuomba radhi kwa chama hicho ndani ya saa 12 kuanzia jana alasiri kilipotoa notisi kwa taasisi hiyo.

Mwenyekiti wa CMPD, Michael Massawe, aliwaambia waandishi wa habari kuwa chama hicho hakitambui kuwapo taasisi hiyo kwa kuwa hakijawahi kushiriki wala kuhusishwa katika kuanzishwa kwake.

"Kwa watu hao kujitambulisha kama wanafanya uangalizi wa CMPD, ni upotoshaji wenye nia ovu ya kuleta mkanganyiko na hasara kwa wanachama wetu wa CMPD.

"Ifahamike kwamba tayari tumepokea taarifa nyingi kutoka kwa wanachama wetu ambao wamekuwa wakijikuta katika sintofahamu kutokana na taarifa zinazotolewa na hii taasisi huku wakiwataja wanachama wetu kama sehemu ya wahusika wa mipango yao wakati si kweli," alisema.

Taarifa hiyo ya CMPD imekuja siku chache baada ya taasisi hiyo kutoa taarifa kupitia moja ya vituo vya runinga nchini kuhusiana na ujio wa kongamano la elimu ya usalama barabarani huku wakikitaja chama hicho cha CMPD kuwa miongoni mwa vyama vilivyomo ndani ya taasisi yao.

"Kitendo cha hawa kututambulisha kama wanachama wao na kuthibitisha ushiriki wetu katika matukio yao, mbali na kuleta mkanganyiko kwa wanachama wetu pia wanatuingiza katika migongano na wadau wetu mbalimbali ambao tayari tupo nao katika makubaliano ya kiutendaji yanayoongozwa kisheria.

"Kupitia wadau hawa, tayari tuna kalenda ya matukio yetu muhimu. Sasa wanaposikia tunahusishwa na matukio mengine bila wao kuwa na taarifa inawasababishia sintofahamu na kutishia makubaliano yetu," alifafanua.

Katika kuthibitisha hatua hiyo, Massawe alisema tayari chama hicho kimeandaa notisi ya kisheria kupitia mwanasheria wa chama hicho, Kampuni ya Uwakili ya Msando Law Office ikiitaka taasisi hiyo kuwaomba radhi wanachama wa CMPD kwa madai ya kutumia vibaya jina la chama chao bila kuwapo makubaliano ya kisheria.

Tangu usajili wake hadi sasa, CMPD ina wanachama zaidi ya 40,000, wakiwa chini ya vituo 1,600 vilivyorasimishwa na serikali kupitia Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Saalam na wataalam kutoka ofisi za halmashauri zote za mkoa huo.



# Wananchi kujenga wodi ya mama na mtoto

**Na Godfrey Mushi,** ARUSHA

WANANCHI wa Kijiji cha Irkaswa, Kata ya Kamwanga, Tarafa ya Enduimet, Wilaya ya Longido, walioongoza kuchangia kutoa ardhi yao kwa asilimia 88.5 kwa ajili ya shughuli za uhifadhi wa ushoroba wa kitendeni, wameazimia fedha zitakazopatikana zijenge jengo la wodi ya mama na mtoto.

Fedha hizo zinazotokana na Mradi wa Wildlife Credit (tuzo ya uhifadhi) unaotekelezwa na Shirika la World Wildlife Fund (WWF). Zahanati ya Irkaswa, ambayo ina wastani wa kutoa huduma za uzazi kwa wajawazito sita kwa siku, haina jengo maalum kwa ajili ya huduma hiyo na wajawazito wanazalia chini kutokana na kukosa vitanda na wodi.

Juzi, katika Mkutano Mkuu Maalum wa kijiji hicho, ulioitishwa kwa ajili ya kupokea na kuupitisha mradi mpya wa majaribio chini ya mradi mkuu, Ofisa Mtendaji wa Kijiji, Paul Lindita, alisema wakipata fedha hizo wataanza na changamoto hiyo kwa wajawazito.

Mradi huo unalenga zaidi kutoa motisha ya utunzaji na ulinzi wa ushoroba wa Kitendeni, ambao ni mapito ya wanyamapori wanaohama kati ya Hifadhi ya Taifa Kilimanjaro (KINAPA) na Hifadhi ya Taifa ya Amboseli ya Kenya kwa ajili ya kutafuta malisho na maji.

"Tatizo letu kubwa hapa hatuna nyumba za watumishi na jengo la mama na mtoto na wananchi hali yao ni mbaya kiuchumi," Lindita alisema.

Mganga Mfawidhi wa Zahanati ya Irkaswa, Dk. Debora William, alishauri kipaumbele cha kwanza kiwe jengo hilo la mama na mtoto.

"Mnafahamu wingi wa watu wanaokuja usiku pale Zahanati, hasa wajawazito, tunazalisha watu mpaka sita kwa wakati mmoja. Jengo la mama na mtoto liwe ni kipaumbele chetu," alisisitiza Dk. Debora.

Mshauri wa Biashara wa WWF na Meneja Mradi huo, Frank Damson, alisema: "Tuna mradi mpya, ambao tumekuja kuuzindua kama majaribio, tutautekeleza katika vijiji vinne vilivyoko katika ushoroba wa Kitendeni.

"Kata ya Kamwanga itanufaika na vijiji vitatu vya Irkaswa, Kamwanga na Kitendeni na Kata ya Olmolog itanufaika na kijiji kimoja cha Lerang'wa," alisema.

Alibainisha kuwa lengo la mradi ni kuhakikisha wanalinda ushoroba wa Kitendeni ambao unaunganisha Hifadhi ya Taifa ya Amboseli na KINAPA.

"Tunaulindaje? Kuna njia tofauti tofauti tutatumia katika miezi 18 ya utekelezaji wa huu mradi wa majaribio. Ukifanikiwa utakuwa kama mfano ambao utakwenda kutumika katika shoroba zingine zote nchini," alisema.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Kamwanga, Anthony Mtae, alisema katika kijiji chao wananchi wameazimia fedha zitakazopatikana kutokana na mradi huo, zitumike kutatua kero ya maji inayowatesa zaidi ya wananchi 10,000 wa eneo hilo lililoko mpakani mwa Kenya na Tanzania.

"Maji yaliyoko huko yanatumika kutoka huduma kwa zaidi ya wananchi 10,000 na watu wanaongezeka, yatatutosha wote? Ndio maana kuna mgawo wa maji, leo Nakilongosi, kesho yake yako Murtoti, siku nyingine yako Mlimani Park, shuleni hayapo," alisema.



Daktari wa Watoto katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Tanga-Bombo, Dk. Mwalimu Khalid, akitoa mafunzo maalumu yanayohusu matibabu ya utapiamlo kwa wataalamu mbalimbali kutoka Ustawi wa Jamii, madaktari, manesi na maofisa lishe wa hospitali hiyo jana. **PICHA: OSCAR ASAENGA**

# DC aonya wananchi kilimo cha bangi

**Na Allan Isack,** ARUMERU

MKUU wa Wilaya ya Arumeru, mkoani Arusha, Emmanuela Kaganda, amewataka wananchi wanaojishughulisha na kilimo cha bangi, kuacha mara moja, vinginevyo serikali itataifisha mashamba yao.

Emmanuela alitoa onyo hilo jana wakati wa operesheni maalum ya kutokomeza kilimo cha bangi katika Kijiji cha Kisimiri Juu. Ni operesheni ya kitaifa ya kupiga vita na kutokomeza biashara na matumizi ya dawa za kulevya nchini.

Akiongoza operesheni hiyo akiambatana na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya hiyo, waliteketeza magunia 270 ya bangi na kilogramu 300 za mbegu na kuwakamata watuhumiwa wanne.

Kiongozi huyo pia alisema amesikitishwa na kitendo cha baadhi ya wananchi kijijini huko kufuta namba za anwani za makazi katika nyumba zao, jambo ambalo linafanya kushindwa kutambua mmiliki wa nyumba ambazo magunia ya bangi yalikutwa ndani ya majengo yao.

Alisema mkakati wa serikali kwa sasa ni kurasimisha mashamba yote ya wananchi wa kijiji hicho kwa kutoa hatimiliki ili kuwatambua wamiliki halisi wa mashamba na hivyo kusaidia kutambua watu wanaolima bangi.

"Serikali kupitia Mamlaka ya Kudhibiti Dawa ya Kulenya imekuwa inatoa elimu kwa wananchi kuacha kulima bangi lakini bado wapo baadhi wanaokaidi.

"Tumekamata magunia 270 na kilogramu 300 za mbegu za bangi, jambo ambalo linaashiria kuwa bado kilimo hicho kinafanyika katika vijiji vya Kisismiri Juu na Losinoni Juu," alisema kiongozi huyo.

Mwakilishi wa Kamishna wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Ofisa Operesheni, Jackson George, alisema licha ya kutoa elimu, baadhi ya wananchi wa Kisimiri wanaendelea kulima na kuuza bangi kwa siri.

Alisema serikali itaendelea na mpango mkakati wa kutoa elimu na kuchukua hatua kali za kisheria kwa mtu yeyote atakayebainika.

# Teknolojia ya kilimo yatiliwa mkazo Arusha

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

KATIBU Tawala Msaidizi, Uchumi na Uzalishaji Mali Mkoa wa Arusha, Daniel Loiruck, amesema kuna umuhimu kila mkulima kutumia teknolojia za kisasa zinazotengenezwa na sekta tofauti za kilimo ili kuongeza mnyororo wa thamani kwenye mazao.

Katika maonesho ya kilimo biashara jijini hapa yaliyoandaliwa na Kituo cha Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), Loiruck, alisema jana kuwa wakifanya hivyo, watanufaika kwa kupata mazao yenye tija na kuwakwamua kiuchumi.

Pia alisema wataepuka magonjwa ya kushambulia mazao yao, kwa kuwa watapata elimu ya kufahamu mbinu bora za kuyadhibiti na kuwa na matumizi sahihi ya viuatilifu na pembejeo.

Loiruck alishukuru sekta binafsi kwa kushirikiana na vituo vya utafiti katika kusambaza teknolojia mbalimbali za kilimo pamoja na matumizi sahihi ya mbolea.

Mkurugenzi Mkuu wa TARI, Dk. Godfrey Mkamilo, aliwataka wakulima kujenga utamaduni wa kutumia matokeo ya utafiti, ili yawasaidie katika ukuzaji wa mazao yao na kuvuna kwa tija.

"Maonesho haya kwa wakulima yanaongeza uchumi wao, yanaleta fursa ya uboreshaji kilimo biashara," alisema.

Wakulima Dorcas Ayo na Suleiman Juma kutoka mkoani Kilimanjaro walilalamikia madhara ya sumukuvu yanayowapata, ilhali wataalamu wa kilimo wako katika kila kata.


Walisema wataalamu hao hawatoi elimu zaidi ya upimaji wa udongo, matumizi ya upigaji dawa mashambani na viuatilifu.

Walisema kuna wakati wanaacha mazao yao yaliwe na wadudu kwa sababu ya gharama kubwa ya kununulia viuatilifu, inayotozwa na wauzaji wa maduka ya pembejeo.

"Tunaomba serikali ifanye utafiti wa wadudu wanaoleta madhara katika mimea. Suala la sumukuvu watafiti watoe majibu sahihi kwetu sanjari na upimaji wa udongo ili watusaidie," aliomba Dorcas.

Mmoja wa watafiti wa Kampuni ya Intacrom, Soma Said, aliomba wakulima kutumia mbolea za Fomi inayorutubisha udongo na kuwawezesha kuvuna kwa tija.

Alisema mbolea hiyo ipo aina tatu; ya kupandia, kukuzia na kunenepesha, akiwashauri wakulima waitumie kwa wingi.



# Mradi bil. 3/- kuondoa kero maji Sengerema

**Na Elizabeth Seleman,** SENGEREMA

SERIKALI mkoani Mwanza imetia saini mkataba wa ujenzi wa tangi la maji la Nyamazungo pamoja na upanuzi wa mtandao wa bomba wenye urefu wa kilomita 73 katika Wilaya ya Sengerema wenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni tatu.

Mradi huo unatarajiwa kuondoa adha ya upatikanaji wa majisafi na salama katika kata saba wilayani hapa.

Mkataba huo umetiwa saini baina ya Serikali na kampuni ya Nangh'were Mhando Ltd na ujenzi wake ukitarajiwa kufanyika katika kipindi cha miezi sita kuanzia Agosti, mwaka huu mpaka Januari, mwakani 2024 na unakadiriwa kuhudumia zaidi ya wananchi 166,500.

Akizungumza wakati wa utiaji saini utekelezaji wa mradi huo, Katibu Tawala wa Mkoa wa Mwanza, Elikana Balandya, aliwataka viongozi kusimamia kikamilifu na kutoa ushirikiano mradi huo utekelezwe katika viwango vinavyotakiwa.

Meneja wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Sengerema (SEUWASA), Sandala Sadiki, alisema mradi huo unatarajia kuwafikia wananchi zaidi 166,500 na utagharimu Sh. bilioni tatu hadi kukamilika.

Alizitaja kata zitakazonufaika na mradi huo kuwa ni Nyamazugo, Ibondo, Tabaruka, Nyatukala, Misheni, Nyampulukano na Mwabaruhi.

Mkuu wa Wilaya ya Sengerema, Senyi Ngaga, aliahidi kuendelea kuisimamia kikamilifu miradi inayotekelezwa wilayani hapa na kuhakikisha hakuna hujuma yoyote inayojitokeza ili kuhakikisha kila mwananchi anapata huduma stahiki.

Mbunge wa Sengerema, Tabasamu Khamis, alionya baadhi ya wananchi wenye utaratibu wa kujiunganishia maji kinyemela na kueleza kuwa hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yao kwa kuwa hawatakuwa tayari kuvumilia vitendo hivyo vya hujuma.

Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Sengerema, Mark Makoye, aliishauri SEUWASA kuangalia kwa makini suala la maji kukatika mara kwa mara kwa kuwa limekuwa kero kwa wananchi.




Viongozi wa Kata ya Matongo katika Halmashauri ya Wilaya na Tarime wakifurahi pamoja na walimu wa Sekondari ya Matongo kwenye hafla ya kukabidhiwa nyumba ya mwalimu wa shule hiyo iliyojengwa na kampuni ya ukandarasi katika mgodi wa Barrick North Mara ya Swala Sulutions kwa kushirikiana na mgodi huo. Wengine ni Kaimu Meneja Uendeshaji wa Kampuni ya Swala Sulutions, Roy Kiprono Kimutai (wa nne kushoto) na Kaimu Meneja wa Idara ya Uhusiano wa Barrick North Mara, Hermence Christopher (wa nne kulia). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TFS yawaangukia viongozi ulinzi rasilimali misitu

**Na Vitus Audax,** NYAMAGANA

WAKALA wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) Kanda ya Ziwa imewataka viongozi mbalimbali wa serikali kushiriki kikamilifu katika kulinda na kuhifadhi rasilimali za misitu na kuacha kulitelekeza jukumu hilo kwa wakala pekee.

Kamanda wa Uhifadhi TFS Kanda ya Ziwa, Bakari Mohamed, alitoa rai hiyo juzi wakati akikabidhi mbao 250 kwa niaba ya Kamishna wa Uhifadhi wa TFS, Prof. Dos Santos Silayo, kwa Mkuu wa Wilaya Nyamagana, Amina Makilagi, kwa ajili ya utengenezwaji wa madawati.

Mohamed alisema kumekuwa na utaratibu wa baadhi ya viongozi kupuuzia pale wanapoona uharibifu wa misitu na kuliona jukumu hilo kuwa si lao bali la TFS hali ambayo imesababisha hali ngumu katika utekelezaji wa majukumu yake.

"Hizi rasilimali za misitu ni kwa faida ya viongozi wote kuanzia vitongoji na wananchi wao. TFS tumepewa tu jukumu la kusimamia lakini sehemu ambao hatupo wanatakiwa kuwa mabolozi ili iendelee kuwahudumia," alisema.

Pia alisema pale wanapogundua kuwapo kwa waharibifu wa rasilimali hizo wasisite kuchukua hatua za kisheria ili kuhakikisha wahusika wanaendelea kudhibitiwa na kulinda misitu.

Alitaja misitu kuwa ni miongoni mwa rasilimali zinazithaminiwa duniani ikiwa ni pamoja na vigezo vinavyeweza kulipa nafasi taifa katika kupatiwa fursa mbalimbali kutoka katika mataifa yaliyoendelea.

Akizungumza baada ya kupokea mbao hizo za miti ya aina mbalimbali ya asili, Makilagi aliishukuru TFS kwa kupokea maombi yake ya mbao kwa ajili ya kutengeneza madawati hali itakayosaidia kupunguza tatizo la samani hizo wilayani hapa.

"Mbao hizi zenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni nne zitasaidia kuongeza madawati katika shule mbalimbali hususani katika shule za msingi. Tunaahidi kuendelea kuwa mstari wa mbele katika kushirikiana na TFS kutunza mazingira ikiwa ni pamoja na kuendelea na kampeni ya upandaji miti kwa wingi," alisema Makilagi.

# Waomba mabwawa kuongeza uzalishaji

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAKULIMA kutoka Halmashauri ya Ushetu, Kahama mkoani Shinyanga, wameishauri Wizara ya Kilimo kuchimba visima virefu na mabwawa ya maji kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji ili kuongeza uzalishaji na kuondokana na dhana ya kutegemea mvua kila msimu.

Hayo waliyabainisha jana katika kikao cha Baraza la Wazazi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) cha kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa shughuli za maendeleo kwa kipindi cha miezi sita kuanzia Januari hadi Juni, 2023.

Walisema serikali ikielekeza nguvu katika kilimo hakutakuwa na ukosefu wa chakula wala malalamiko ya wananchi, hivyo kuna haja ya kuwekeza katika uchimbaji wa mabwaya ya maji yatakayosaidia katika kilimo cha umwagiliaji.

"Visima virefu na mabwawa ya maji yakichimbwa yatasababisha wakulima kuzalisha kwa wingi mazao ya chakula na biashara na wataondokana na dhana ya kuendelea kutegemea mvua za kila mwaka," alisema Ahmed Haruna.

"Msimu uliopita nilinunua ekari 10 nje ya mji kwa ajili ya maandalizi ya kilimo. Kutokana na mvua kuwa chache nilivuta maji katika moja ya maghati ya maji yanayosimamiwa na RUWASA (Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini) na kulima matunda. Mavuno yalikuwa mengi, hivyo kuna haja ya serikali kulitazama hili," aliongeza.

Makamu Mwenyekiti wa Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Ushetu, Doa Limbu, alisema halmashauri hiyo inategemea mapato yake ya ndani kupitia kilimo, hivyo uwapo wa kilimo cha umwagiliaji utasaidia kuongeza mapato ya ndani na kuwa na fedha za ukamilishaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo na ile iliyoanzishwa kwa nguvu za wananchi.

Mbunge wa Ushetu, Emmanuel Cherehani, alisema moja ya mikakati yake ya kukuza kilimo ni kuwa na kilimo cha umwagiliaji ili kuongeza uzalishaji wa mazao hayo na kitaanza hivi karibuni baada ya upatikanaji wa maji ya Ziwa Victoria ambayo yanatarajia kuingia jimboni humo.

Alisema, kwa kuona umhimu wa kilimo cha umwagiliaji, Chama Kikuu cha Ushirika Kahama (KACU) kwa kushirikana na Halmashauri ya Ushetu wamepanga kuchimba mabwawa 11 ya maji ili kukabiliana na ukame kwani msimu ulipita baadhi ya makambuni ya tumbaku yalikuwa yakisomba maji na kuwapelekea wakulima.




Ukurasa 13

‘Cheti cha ndoa hakisainiwi wakati wa uchumba’



## Kariakoo ‘kuchele’ ni mambo yanayojiri baada mkutano wa Waziri Mkuu Majaliwa

Ukurasa 12

BUFE
IJUMAA JULAI 21, 2023
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

# Vyanzo vuta nikuvute, kushindwa kurejesha mikopo kumbe viko hapa

**Na Christina Haule, MOROGORO**



MIGOGORO kati ya wakopaji na taasisi za fedha zinazokopesha inazidi kukua kila siku, huku visa vyake vikiwa kutozwa riba kubwa, kufilisiwa, kuvunjika kwa ndoa kwa upande mmoja na hasara kwa taasisi baada ya aliyekopa kuingia mitini, vikisikika mara kwa mara.

Aidha, wakopaji mikopo kushindwa kulipa hasa baadhi ya kinamama wajasiriamali ni jambo linaloshika kasi huku baadhi yao wakitokomea kusikojulikana na kuziachia hasara taasisi zinazotoa mikopo na hata familia zao.

Haya yanatokea licha ya kuwapa elimu na mbinu za kutumia kwa tija pesa hizo wanazokopa ili kukuza mtaji au kuboresha biashara.

Changamoto ya wakopaji wengi wa mikopo kushindwa kulipa mikopo na riba kulingana na muda uliopangwa inahusishwa na baadhi yao kuiingiza au kutumia pesa hizo kutatua changamoto za maisha kwenye familia zao badala ya uwekezaji.

Mathalani, wapo wanaokopa kutibu wagonjwa, wengine kununua mahitaji yasiyo ya lazima na baadhi kutumia fedha hizo, kulipa mkopo mwingine waliokopa kwenye taasisi nyingine.

Tabia hiyo, inaweza kuwa ni kinyume na kanuni za mikopo kwa vile haijatimiza lengo na kusudi lilikuwepo.

Jonas Laurent ni mmoja wa wajasiriamali ambaye ni mkulima wa mboga na matunda anayeishi Dumila wilayani Kilosa mkoani Morogoro, anayeeleza hayo wakati akiongea na Nipashe.

Anafafanua kuwa upo ukweli kwamba kuitumia mikopo kutatua changamoto za kimaisha na kifamilia kunatokana na hali ya umaskini na mitaji midogo ya wajasiriamali ambayo haitoshi kukidhi mahitaji ya familia na wategemezi.

Anaitaja sababu nyingine kuwa ni kutumia fedha hiyo katika kurejesha mikopo iliyokopwa kwanza na baadaye kushindwa kurejesha aliyokopa na ndipo hufikia hatua ya kukomolewa na mkopo wa kausha damu, kufilisiwa na kujikuta wakiua mitaji na biashara wakibaki bila mwelekeo.

“Inawezekana mjasiriamali kwa wakati huo hahitaji mkopo wa biashara lakini ana mtoto au ndugu yake wa damu anaumwa na anahitajika fedha nyingi kuokoa uhai wake, analazimika kuingia mkopo mwingine ili kunusuru maisha ya mpendwa wake. Sasa shida inakuja kwenye kulipa, hadi waanze kuvutana na ndugu wengine, huku riba nayo inaendelea kukua,” anasema Laurent.

Wakati mwingine anashindwa kulipa, anaweza kukimbia kusikojulikana au hata kujinyonga na pengine wapo wanaoachilia mali zao na kufilisiwa.

Meneja wa taasisi ya kiserikali ya utoaji mikopo ya Self Microfinance Fund (Self MF), tawi la mkoa wa Morogoro, Moses Ntambi, anatoa rai kwa vyombo vinavyosimamia warasimishaji na ardhi kuongeza kasi ya urasimishaji maeneo ili kuwafanya wakopaji kuwa na dhamana.

Anazitaja nyaraka za mali zilizorasimishwa zenye namba kwamba wanazoweza kuzitumia kupata uhakika wa mkopaji kama hana mkopo mwingine ili kumkopesha bila mashaka.

Aidha, anasema urejeshaji hafifu au kushindwa kurejesha mikopo kutafanya juhudi za serikali kuwasadia wananchi kutozaa matunda ikiwa bado kutakuwa na wajasiriamali wanaokopa mikopo na kisha kupotea na kushindwa kulipa.

Hata hivyo, anasema mkopaji anaposhindwa kulipa inakuwa shida kwa mtoaji wa fedha kuipata dhamana aliyokopea kutokana na kuwa tayari ipo katika mikopo kwenye maeneo mengine zinakopatikana huduma hizo.

Anasema licha ya taasisi hiyo kujenga utaratibu wa kutoa elimu kabla ya mikopo kwa wajasiriamali mbalimbali wakiwamo wakulima, wafanyabiashara, wafanyakazi na wafugaji kuhusu muda wa utayari wa kukopa kulingana na biashara waliyonayo, bado changamoto hiyo imeendelea kushika kasi.

Kadhalika, anawashauri wajasiriamali kuzingatia elimu wanazopewa hasa za masuala ya mikopo ili kutojiingiza kwenye mikopo umiza ambayo ina mchango mkubwa wa kuwaharibia maisha na uwekezaji kwa sababu ya kukimbia na kuacha shughuli za maendeleo wanazofanya, ili kujiepushia matatizo.

Halikadhalika, Ntambi anasisitiza taasisi nyingine za kifedha kutumia mfumo wa taarifa za wakopaji mikopo uliopo serikali (credit bureau) katika kuweka maelezo ya wateja wa mikopo na kusaidia watoa huduma wengine kuwatambua na kutowapa fedha nyingine watu ambao wameshakopa kwingine na wapo kwenye orodha.

Ofisa Mikopo wa Self MF, Faraja Kauzeni, kwa upande wake anasema mikopo inayotolewa na taasisi hiyo ya kiserikali ina lengo la kuwainua wananchi kiuchumi kutoka hatua moja kwenda nyingine na inasikitisha kama haitatumiwa ipasavyo.

Hivyo Kauzeni anawashauri wajasiriamali na wafanyabiashara kufika kwenye taasisi hiyo kupata elimu zaidi ya namna ya kuendesha biashara zao na kwamba Self MF ina uwezo wa kumsaidia mjasiriamali kielimu na kumfahamisha kuwa ni wakati gani anatakiwa kukopa au wakati gani asikope ili kuepuka kutokuwa na iwezo wa kumaliza mkopo.

Anaongeza kuwa taasisi ya Self MF imetoka mikopo yenye thamani ya Shilingi bilioni mbili kwa wateja 120 mkoani Morogoro tangu tawi hilo lifunguliwe mwaka 2022.

## BIASHARA

# Kariakoo ‘kuchele’ ni mambo yanayojiri baada mkutano wa Waziri Mkuu Majaliwa

•Wafanyabiashara wasema kila kona ni shwari, watia neno mkataba bandari



Waziri Mkuu Kasimu Majaliwa , kwenye mkutano na wafanyabiashara Kariakoo.

**Na Halfani Chusi**

MAMBO yamebadilika kwa wafanyabiashara kuanzia Kariakoo hadi mikoa mingine nchini, ndivyo anavyojinasibu Katibu wa Jumuiya ya Wafanyabiashara Kariakoo, Urokh Ombeni.

Akiihusisha amani na furaha walionayo wafanyabiashara hao na mkutano wa Waziri Mkuu, Kasimu Majaliwa na wafanyabiashara Kariakoo kutatua kero zao baada ya mgomo wa kupinga ongezeko la kodi.

Ni katika mazungumzo na Nipashe hivi karibuni akisifia ziara ya Waziri Mkuu na Rais Samia, Suluhu Hassan kukubali na kuwaita wafanyabiashara na kufanya nao mkutano wa pamoja kwa lengo la kusikiliza na kutatua kero zao kwa nyakati tofauti.

Ikumbukwe kuwa, Mtendaji Mkuu wa serikali alifikia uamuzi wa kukutana na wafanyabiashara wa Kariakoo baada ya mgomo wa siku tatu mfululizo wakidai kuongezwa kodi na madai mengi yanayokata mitaji yao na kuwadhoofisha kibiashara ikiwamo kodi ya stoo.

### HALI ILIVYO SASA

Katibu wa Jumuiya ya Wafanyabiashara Kariakoo, Urokh, anasema tangu Waziri Mkuu, atoe maagizo hayo kwa sasa hali imekuwa shwari na wafanyabiashara wanaishi kwa amani na wanalipa kodi bila bughudha yoyote.

“Hali ya biashara imetulia sasa hivi watu wanafanyakazi kwa utulivu mkubwa, ila tulikuwa tunatamani kuwe na bei elekezi ya kutoa kontena bandarini ili mtu akienda kuchukua shehena hiyo ajue anapaswa kulipia Shilingi ngapi kuliko hili la kukaa na baadhi ya maofisa kuanza kujadiliana ni kama hili linakaribisha mwanya wa rushwa.

“Zamani walikuwa wanatusumbua sana tulikuwa tunafanya biashara bila kuwa huru kila mara unawaza kikosi kazi, wakati mwingine unawaza TRA watakuvamia dukani.

“Tunamshukuru Waziri Mkuu na Rais Samia kwa kujali malalamiko yetu na kututembelea lakini tunatamani angalau angekuwa wanafanya ziara hiyo kila baada ya miezi kadhaa. Nadhani kusingejitokeza suala kama lile tena,” anasema katibu huyo.

### KUHUSU BANDARI

Katibu huyo pia anaunga mkono uamuzi wa serikali kuhusu kukodisha bandari kwa mwekezaji DP World kutoka Dubai, akitoa mtazamo wake kwamba atakapokuja huenda ataleta maslahi kwa wafanyabiashara ikiwamo kuondoa kikwazo cha kukaa kontena muda mrefu bandarini na mazingira ya rushwa na ukwepaji kodi.

Anasema mpango huo ni mzuri lakini ana angalizo kwamba, kuwapo na ungalifu kwenye mkataba usiwe wa kuwabana Watanzania bali wenye manufaa kwa pande zote au ‘win-win’ lakini pia ukimlinda mwekezaji ili kila upande upate tija na nchi ineemeke na hatua hiyo.

“Ni jambo zuri kwa vile litafanikisha kuondoa vikwazo kwa wafanyabiashara na mianya ya rushwa lakini uangaliwe mkataba kama kuna sehemu inatubana kama taifa, basi maeneo hayo yarekebishwe mapema na kuleta mlango wa mijadala kuridhiana,” anashauri.

### KARIAKOO SASA

Baada ya mkutano huo Nipashe inashuhudia, pilikapilika zikiongezeka katika soko hilo, wingi wa wafanyabiashara umeonekana wakiwamo wageni kutoka DRC, Burundi, Comoro, Kenya na baadhi wageni wanaoleta shehena kutoka China na Uturuki.

Mitaa ya Congo na Sikukuu imekuwa na msongamano mkubwa kama ilivyokuwa hapo zamani, hali inayoifanya safari ya Kariakoo kuhitaji umakini zaidi kwenye pochi mifukoni, fedha na hata simu mkononi.

Wanamgambo wanaolinda usalama wapo lakini siyo wengi kumudu tafurani au kama kutatokea vurumai kutokana na idadi kubwa ya watu.

Vijiwe vya watu wasio na kazi maalumu pamoja na madalali wa kusaka bidhaa nao wameongezeka na kusababisha kero kwa wateja wanaofuata huduma hizo ikiwamo kuongeza bei za bidhaa ili wapate cha juu lakini pia kusumbua wateja hasa wageni na kuongeza hofu ya kuibiwa kutokana na kusongwa na watu hao mara kwa mara.

### KUZUKA MGOMO

Mgomo wa wafanyabiashara Kariakoo uliitikisa serikali na hata Waziri Mkuu akaunda tume iliyozunguka nchi nzima kwa ajili ya kusikiliza kero za wafanyabiashara na kuzileta mezani kwa utatuzi.

Mkutano wake na jumuiya ya wafanyabiashara, unaanza na kutoa ufumbuzi wa mambo kadhaa ambayo anayatolea ufafanuzi kwenye mkutano wa hadhara na wafanyabiashara ambao wanakubaliana nayo.

Miongoni mwa kero anazotatua papo kwa hapo ni pamoja na tuhuma dhidi ya baadhi ya maofisa wa Mamlaka ya Mapato kuwaonea baadhi ya wafanyabiashara kwa kuwatolea maneno ya kashifa na kutowasilikiza wanapowasilisha malalamiko yao kwa madai mpaka waone barua rasmi.

Kuhusu sheria ya usajili wa stoo, ambayo ndicho kilikuwa kiini cha mgomo huo, siku hiyo akaelekeza sheria hiyo kutotumika kwa muda mpaka pale itakapotolewa elimu kwa wafanyabiashara.

“Sheria ya usajili wa stoo ilikuwa na nia njema, lakini imeanza kutumiwa bila kutoa elimu hivyo naagiza isitishwe kwanza kuruhusu zoezi la utoaji wa elimu kuendelea huku wakiangalia namna bora ya kulitekeleza agizo hili.”

Vilevile suala la rushwa linaibuliwa na wafanyabiashara wakidai wanabambikizwa kodi kubwa na hata kutishiwa kufunguliwa kesi za uhujumu uchumi, lakini ‘wanapolainisha’ kwa kutoa kitu kidogo, mambo yanamalizwa. Waziri Mkuu anakemea rutoa mlungula kwa baadhi ya maofisa wa Mamalaka ya Mapato akiwaeleza kuwa ni kosa kisheria kupokea rushwa na kwamba jambo hilo linasababisha wafanyabiashara kuendelea kubaki maskini.

“Mbali na rushwa hata kamatakamata hakuleti sifa nzuri mnakamata mpaka wateja wa nje wanaokuja kununua bidhaa kitendo hicho kitasababisha kufukuza wateja wa kigeni. Kumbukeni soko la hili linategemewa na nchi tunazopakana nazo kama Kongo, Rwanda, Burundi kumkamata mtu na kumtisha kutatufukuzia wateja wetu na tutakosa fedha za kigeni kutoka nje,” alisema siku alipoenda kusikiliza na kutatua kero za wafanyabiashara Kariakoo.

Kadhalika anaagiza kufutwa kwa vikosi kazi vilivyoundwa na TRA, akisisitiza kuwa hivyo ndiyo sababu ya rushwa kati ya wafanyabiashara na serikali huku akiahidi kuwa hawatakubali soko la Kariakoo kufa.

“Tutwasaidia wafanyabiashara kutatua kero zinazowakabili, tutafanya mkutano na viongozi wao kwa ajili ya kupokea malalamiko na maoni yao, kuangalia namna ya kuyafanyia ufumbuzi kwa pamoja.”

Pia anaahidi atafanya mkutano na viongozi wa wafanyabiashara wote nchini, Jumatano kwa ajili ya kupokea vikwazo vinavyowakabili na kuvitafutia ufumbuzi wake.



Katibu wa Jumuiya ya Wafanyabiashara Kariakoo, Urokh Ombeni.**PICHA ZOTE : HALIFANI CHUSI**

## TAFAKURI YA MLALAHOI

# ‘Cheti cha ndoa hakisainiwi wakati wa uchumba’






**NA JOSEPH KULANGWA**
Simu: +255 713 410008
barua pepe: kulangwasos@gmail.com

BANDA ni mtoto wa kiume wa familia ya Mzee Tandu Uweke. Siku moja wawili hao wakafanya safari mkoani, kwa masuala yao binafsi na kupokewa na ndugu na jamaa kwa bashasha.

Katika siku walizokaa mkoani humo, Banda akavutiwa na msichana anaitwa Dupwo Mwarabu, hali iliyomfanya atamani kumwoa na hakusita kumwambia baba yake.

Mzee Tandu hakuwa na hiyana, akamkubalia kijana wake kutokana na kwamba hata umri wake ulishafikia haja ya kuwa na mke na kuishi kama familia.

Hata hivyo, katika njia zao, Banda na Dupwo kumbe kuna siku walikutana na ndipo mwanaume huyo akafunguka, na bahati nzuri msichana naye hakuwa na pingamizi akamtaka afuate tu taratibu.

Kwa maana hiyo, baada ya Banda kupata ruhusa na idhini ya baba yake, akajiweka tayari na kumtaka mzee wake huyo aanze taratibu za kuhakikisha wawili hao wanaoana.

Kimila taratibu ni kufuatilia ukoo wa bibi harusi mtarajiwa, ili kuujua vema na kama kuna dosari au upungufu wajipime kama wanaweza kukabiliana nao, na kama ni kubwa basi mambo yaishie hapo.

Kwa kuwa Mzee Tandu alikuwa analifahamu vema eneo hilo na akiwa na watu anaofahamiana nao, aliwaomba baadhi yao kufuatilia ukoo wa Mzee Mwarabu, ili mwanawe asijeangukia kwenye familia ya ajabu.

Wakati shughuli hiyo ikiendelea ya utafiti, Banda na baba yake walirudi nyumbani kusubiri matokeo, huku yeye akiendelea kuwasiliana na mkewe mtarajiwa.

Utafiti ulikamilika na ikaonekana kuwapo mambo madogo madogo tu yanayoweza kurekebishwa, kabla ya ndoa haijafungwa. Yalirekebishwa na hatimaye maandalizi ya ndoa baina ya familia hizo mbili yakaanza.

Hatua hiyo ilifikiwa baada ya pande hizo kuchunguzana kwa nyakati tofauti na zote kuridhika na kuridhia ndoa ifungwe lakini kiserikali, kwa walikuwa na madhebu tofauti.

Hatimaye mambo yakafanyika, watu wakala ubwabwa na kucheza ngoma na kila kitu, Banda na Dupwo wakawa mke na mume, hivyo koo za Tandu na Mwarabu zikaungana kupitia vijana wao na kuleta faraja kubwa.

Endapo Banda na Dupwo wangekimbilia kufunga ndoa bila kuchunguzana pande zote na hatimaye matatizo kuibuka wakiwa wameshasaini vyeti vya ndoa, sijui ingekuwaje, bila shaka hali ingekuwa ya tafrani.

Siku zote masuala ya ndoa ni kama mkataba ambao huingiwa na pande mbili ukiwa na ahadi za kuishi pamoja hadi kifo kiwatenganishe, na ahadi hutolewa siku wanasaini vyeti vya ndoa.

Na kwa kuwa ni mkataba wa milele, ndiyo sababu haiwi vizuri kusaini cheti cha ndoa kabla ya kuridhiana kitabia na nyendo za kila upande kiukoo, vinginevyo ni taharuki.

Ndiyo sababu hata wakati wa kusaini vyeti vya ndoa kunakuwa na mashahidi wa pande zote mbili, wakisaini kwa majina kamili na saini zao na nakala kuachwa serikalini kwa ajili ya rejea.

Hivi sasa nchi inapitia katika mjadala mzito kuhusu uwekezaji katika masuala ya kiuchumi baina ya Serikali ya Tanzania na ile ya Dubai kuhusu bandari za Tanzania kukodishwa kwa kampuni ya DP World.

Kumeibuka ubishaniwa huu ni mkataba au si mkataba, huku wasemao ni mkataba waking’ang’ania saini zinazoonekana kwamba tayari zimehalalisha mkataba ambao wengine wanataka yaitwe makubaliano ya awali.

Kila upande wa serikali ukiibuka na kutoa ufafanuzi na majibu, upande unaopinga unashikilia, kuwa mkataba tayari na hakuna kinachobadilika licha ya viongozi wakuu kusema watasikiliza maoni ya wananchi.

Yawezekana viongozi wetu walikuwa na bado wana nia njema kabisa ya kuwekeza kwenye bandari zetu, lakini kuna mahali walisahau kuwa wakati wa uchumba cheti cha ndoa huwa hakisainiwi.

Kama tungefanya zilivyofanya familia za Tandu na Mwarabu, tusingefika huku tuliko sasa, ambako tunakaribia kutoana macho kwa kinachoonekana ni mkataba uliosainiwa tayari.

Pengine busara itatumika, hatimaye Watanzania tuliofika Dubai na ambao hatujaenda tukakaa pamoja na kuona ni jinsi gani ya kuendelea au kuachana na mchakato huu kwa maslahi mapana ya nchi. Alamsiki!

BIASHARA

# Mgodi ulivyowatajirisha vijana kupitia mradi kilimo biashara



Meneja Uhusiano, Hermece Christopher na Ofisa Maendeleo ya Jamii, Praygod David, wakizungumza na wanakikundi cha kilimo biashara cha mboga na matunda wa Matongo.

**Na Faustine Feliciane**

ILE hali ya umaskini katikati ya utajiri imeanza kutoweka, baada ya mgodi wa dhahabu wa North Mara ulioko wilayani Tarime kuandaa mradi maalum wa kilimo kwa vijana ili kuwatengenezea mapato, kupunguza ufukara na uhalifu.

Hatua hiyo inafuatia miaka kadhaa ya mivutano kati ya vijana wa wilaya ya Tarime Vijijini, uliko mgodi wa dhahabu wa North Mara, unaomilikiwa na Barrick, kutokana na kuingiliana katika shughuli za kutafuta kipato kati ya wananchi hasa vijana na walinzi wa mgodi huo.

Chanzo kilihusishwa na baadhi ya wananchi kuingia kwenye mgodi kusaka mawe ili kuchenjua (kusafisha) dhahabu kwa kuwa shughuli kubwa ilikuwa uchimbaji mdogo wa madini hayo katika eneo hilo, kabla ya kubinafsishwa kwa mwekezaji huyo.

Vijana wengi walikuwa wakiingia kwenye migogoro na mgodi huo kwa sababu waliingia kutafuta mawe lakini askari au walinzi wa mgodi walipambana ili kuwadhibiti na kulinda mali za kampuni.

Katika kutafuta suluhu ya kuepuka migogoro hiyo, uongozi wa mgodi huo uliandaa mradi maalum wa kilimo kwa vijana ili kuwatengenezea mapato kupitia mashamba waliyoyaanzisha kupunguza umaskini wa kipato miongoni mwao.

Naibu Meneja wa Idara ya Uhusiano wa Barrick North Mara, Hermence Christopher, anazungumza na Nipashe, akisema lengo la kuanzisha mradi huo wa kijamii ni kutoa ajira kwa vijana na kuwapa fursa ya kutengeneza pesa kwa njia halali na kuacha kuvamia maeneo ya mgodi huo.

Anasema miradi hiyo ilianzishwa kupitia fungu la miradi ya jamii (CSR) inayotolewa na mgodi huo kwa jamii ya North Mara na kwamba Barrick kwa kushirikiana na Wilaya ya Tarime iliandaa shamba la ekari 10 ambalo wanalima kisasa mboga na matunda ambavyo soko la kwanza la kununua mazao hayo ni mgodi wenyewe kupitia kampuni inayolisha chakula mgodini hapo.

Christopher, anasema lengo la kuanzisha mradi huo wa kijamii ni kutoa ajira kwa vijana na kuwapa fursa ya kutengeneza pesa kwa njia halali ili kumudu maisha yao na kuachana mambo ya kihalifu.

"Mradi huu ulianza mwaka jana, vijana wamejikusanya kwenye vikundi na kukabidhiwa kila kikundi ekari moja ambayo inazalisha mpaka Shilingi 9,000,000 kila wanapovuna na kuuza mazao yao," anasema Christopher.

Aidha anasema, kila kikundi wapo 10 na kufanya idadi ya vijana kwenye mradi huo kuwa 100 na kuongeza: "Tulianza kwa kuwapa elimu ya kilimo cha mboga, ufugaji wa kuku na samaki, baada ya hapo ndipo tukawakabidhi shamba na wataalamu kuwasimamia ili kuleta matokeo chanya na endelevu."

Anasema mwaka mmoja sasa tangu mradi kuanza na vikundi vimefanikiwa kwa kiwango cha juu baada ya kuzalisha mboga nyingi kuliko mahitaji ya kampuni ya kulisha wafanyakazi wa mgodi huo na kupata wateja nje.

"Sasa wana vikundi wanauza mazao yao mengine kwenye soko la nje na wafanya biashara wanayafuata moja kwa moja shambani, Barrick tunanunua asilimia 40 ya mazao yote na nyingine 60 zinazobakia wananunua watu kutoka maeneo mbalimbali," anasema Christopher.

Msimamizi wa mradi huo na Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Barrick, Praygod David, anasema kwa sasa vijana wengi wa maeneo ya Tarime Vijijini hususani Kijiji cha Matongo wameanza kunufaika na kubadilika kiuchumi.

"Hapa vijana na kinamama wanatengeneza pesa nyingi, wapo ambao wamejenga nyumba zao kwa kupitia mradi huu, lakini kubwa na zuri ni vijana sasa kujihusisha na kuvamia mgodi kwani wamejikita kwenye kilimo hiki cha mboga," anasema David.

Anaeleza kuwa vyakula vyote vya mboga na matunda ambavyo vinatumika kwenye mgodi huo wa North Mara vinanunuliwa kwa wakulima hao vijana na unaendelea kufanya vizuri kwa sababu uhakika wa soko upo na pia namna ulivyoandaliwa, hapa wanatumia kilimo cha umwagiliaji ambacho ni cha kisasa na chenye uhakika zaidi.

Anasema Barrick iligharamia kuandaa mradi huo kwa kutengeneza miundombinu ya kujenga kisima cha mita 150 na tangi kubwa la maji wanalolijaza kwa ajili ya umwagiliaji.

"Huko nyuma tulikuwa tunavuta maji kutoka Mto Tigite ambao upo hapa jirani na kuyafikisha shambani, lakini kwa sasa tayari kuna kisima na kazi inayofanyika ni kutengeneza tangi kubwa la kuhifadhai maji," anasema David.

Mmoja wa wanakikundi katika mradi huo, Mlori Kilindo anasema umekuwa mkombozi wao kutokana na fedha wanazotengeneza kuwawezesha kumudu maisha.

Anasema shambani, wanalima mboga kama sukuma wiki, spinachi, kabichi, karoti, vitunguu, nyanya, pilipili, matango pamoja na matunda hasa matikiti maji.

"Hivi vyote tunaviuza mgodini ambao unanunua asilimia 40 na tunatengeneza zaidi ya milioni 30 kwa vikundi vyote 10, mazao mengine sasa hivi kwa sababu tayari tunafahamika wafanyabiashara wanakuja kununua shambani na wao wanayapeleka sokoni, " anasema Kilindo.

Aidha, mkulima mwigine, Felister Mnanka, mkazi wa kijiji cha Matongo anasema mafanikio waliyoyapata wanafikiria sasa kupanua shughuli za mradi huo.

Naibu meneja wa mahusiano, Christopher anasema kutokana na mafanikio ya mradi huo wa Matongo, sasa wapo kwenye mchakato wa kuanzisha mradi kama huo kwenye vijiji vingine vinavyozunguka mgodi

"Awamu ya pili pamoja na kuongeza mradi hapa Matongo, lakini tutaanzisha mwingine kwenye vijiji vya Nyangoto, Nyabuhire na Mjini Kati ili kutoa fursa kwa wananchi kujiinua kiuchumi," anasema Christopher.

Itaanzishwa kwenye mgao ujao wa fedha za miradi ya jamii zinazotolewa na Barrick kwa ajili ya kusaidia maendeleo ya jamii zinazozunguka migodi yake ya North Mara na Bulyanhulu uliopo Wilaya ya Kahama mkoani Shinyanga.



Baadhi ya wanakikundi wakiendelea na kilimo shambani hapo. **PICHA: BARRICK**



## HABARI DODOMA

# Tume yateta na AZAKI adhabu ya kifo

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

TUME ya Kurekebisha Sheria Tanzania (LRCT) imekutana na asasi zisizo za serikali likiwamo Shirika la Reprieve la Uingereza na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) kwa ajili ya kupokea na kubadilishana mawazo namna ya kufanya marekebisho ya sheria kuhusu adhabu ya kifo nchini.

Kaimu Katibu Mtendaji wa LRCT, Geasi Mwaipaja, akizungumza jana mjini hapa katika kikao hicho, alisema tume hiyo itaendelea kupokea mapendekezo kutoka kwa wadau mbalimbali zikiwamo asasi zisizo za kiraia.

Mwaipaja ambaye aliongozana na wanasheria Japhace Daud, Msafiri Shamsi Idd na Zakaria Kegoro, alisema katika sheria ya adhabu ya kifo wamekutana na Reprieve ili kupata uzoefu namna gani wamefanya katika nchi zingine kuhusu kufutwa kwa adhabu ya kifo.

Naye Ofisa Programu Mwandamizi wa LHRC, Raymond Kanegene, alisema sheria ya adhabu ya kifo imekuwa na tatizo kwa kuwa haitoi uhuru kwa majaji kutafsiri sheria, kutoa adhabu mbadala kulingana na kosa lililofanyika na kwa kuzingatia historia au hali ya mtuhumiwa.

Kadhalika, Ofisa Programu wa Reprieve, Linda Kitenge, alisema shirika hilo limekuwa kinara kwa kupigania uhuru wa kuishi kwa kushiriki mijadala mbalimbali inayosaidia kuondoa hukumu ya kifo katika nchi mbalimbali za Afrika zikiwamo Malawi, Kenya na Uganda.

Alisema shirika hilo sasa limeanza kufanya kazi Tanzania kwa kushirikiana na LHRC.

## Wakulima kufikiwa elimu mbegu bora

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

ZAIDI ya wakulima 25,000 katika mikoa ya Dodoma, Morogoro na Singida watafikiwa na elimu ya uzalishaji mbegu bora za mtama na karanga kwenye maeneo yao.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa, Katibu Mtendaji wa Shirika la Wakulima Wazalishaji Mbegu Dodoma (DASPA), Aithan Chaula, alisema wakulima hao watanufaika kupitia mradi wa uzalishaji mbegu bora ngazi ya kijiji unaotekelezwa na kupitia ufadhili wa CIMMYT Mexico chini ya mradi wa AVISA.

Chaula alisema kuwa lengo la mradi huo ni kumwezesha mkulima kuzalisha mbegu ngazi ya kijiji.

"Mradi utawezesha wanawake na vijana kwenye uzalishaji wa mazao ya kawaida na mbegu na kuunganishwa na masoko. DASPA imekuwa ikishirikiana na vituo vya utafiti ikiwamo Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) Naliendele (Mtwara), Ilonga (Morogoro) na Hombolo mkoani Dodoma," alisema.

Alisema wamekuwa wakishirikiana na halmashauri katika maeneo ya utekelezaji wa mradi na Shirika la Udhibiti wa Ubora wa Mbegu (TOSCI) na mashirika yasiyo ya kiserikali ikiwamo Action Aid na shirika lisilo la kiserikali la maendeleo na msaada Waadvesta Wasabato (ADRA).

Aliyataja mashirika ya kimataifa wanayoshirikiana nayo ni Shirika Utafiti wa Mazao Yanayomea Nyanda Kame (ICRISAT) la Malawi na India na Taasisi ya Wafanyabiashara wa Mbegu Tanzania (TASTA) ambao wanasimamia utekelezaji wa mradi.

Chaula alisema kuwa tayari baadhi ya wakulima wameweza kupata mafunzo ya kuwa wazalishaji wa mbegu.

"Tulianza na Chamwino lakini sasa mradi umefikia mikoa mingine ya Singida na Morogoro, haya ni mafanikio makubwa kwetu," alisema.

Alisema wametoa mbegu za mtama katika shule 100 katika wilaya ya Chamwino ili wanafunzi wazalishe mtama kwa ajili ya lishe shuleni.



Wanafunzi wa Shule ya Msingi Bahi Misheni wilayani Bahi wakitoka kukata kuni kwa ajili ya matumizi ya nyumbani jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Vikwazo wenye ulemavu kupata haki polisi, mahakamani vyatajwa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KUKOSEKANA kwa miundombinu rafiki kwenye majengo ya vyombo vya utoaji haki na wakalimani wa lugha ya alama kwa wasiosikia, kumeelezwa kuwa baadhi ya vikwazo kwa watu wenye ulemavu kupata haki zao.

Wadau wa masuala ya walemavu nchini walibainisha hayo juzi jijini hapa wakati wa kikao cha kupitia ripoti ya kuangalia namna watu wenye ulemavu nchini wanavyopata haki katika vyombo vya utoaji haki kilichoandaliwa na Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS).

Mmoja wa wadau hao, Enock Mbawa, akizungumza na waandishi wa habari, alisema watu wenye ulemavu bado wanakabiliwa na kero mbalimbali katika vyombo vya utoaji haki nchini.

"Vyombo vya utoaji haki kama mahakama na polisi bado kuna changamoto mbalimbali kwa watu wenye ulemavu. Kama mlemavu anakesi lakini hana mkalimani wa kumsaidia kutafsiri mambo mbalimbali ya kimahakama lazima ataachana na kesi hiyo, hivyo kupoteza haki yake," alisema.

Aliomba serikali kuwekeza nguvu kwenye miundombinu rafiki kwa watu wenye ulemavu katika majengo yote yanayotumika kutoa haki.

Aidha, aliitaka serikali kutenga bajeti jumuishi ambayo itasaidia makundi ya watu wenye ulemavu nchini kupata haki sawa kama ilivyo kwa wananchi wengine.

Naye Ofisa Ustawi wa Jamii kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, Kitengo cha Watu Wenye Ulemavu, Bruno Mwakibibi, alisema lengo la kikao hicho ni kuangalia kero ambazo wanakumbana nazo watu wenye ulemavu kupata haki kwenye vyombo hivyo.

Alisema bado kuna kero mbalimbali ambazo zinawanyima watu wenye ulemavu kupata haki zao katika vyombo vya utoaji haki ikiwamo miundombinu isiyo rafiki kwao.

Mwenyekiti wa TLS Kanda ya Kati, Mary Munisi, alisema lengo la kupitia ripoti hiyo ni kuisaidia serikali kufanya maboresho katika sheria pamoja na sera mbalimbali ili kuwezesha wenye ulemavu kufikiwa na huduma za vyombo vya utoaji haki nchini.

Mwenyekiti wa Kamati ya Mawakili na Wanasheria Wenye Ulemavu wa TLS, Gideon Mendes, alisema kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022, asilimia 10 ya watu kati ya Watanzania zaidi ya milioni 61 wana ulemavu hivyo wanayo haki ya kupata huduma kama ilivyo kwa wengine.





# DC atangazia vita wanunuzi pareto mbichi

**Na Nebart Msokwa,**
MBEYA

SERIKALI wilayani Mbeya, imezitaka kampuni zinazonunua pareto kuwachukulia hatua mawakala wanaonunua maua ya wakulima ambayo hayajakauka kwa kuwa kufanya hivyo ni kuharibu thamani ya zao hilo.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malisa, alitoa maelekezo hayo kwenye kikao cha wadau wa pareto kilichofanyika katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi kujadili kero mbalimbali zinazolikabili zao hilo.

Kikao hicho kiliwashirikisha wadau mbalimbali wa pareto wakiwamo wakulima, wauzaji wa pembejeo za kilimo, kampuni zinazonunua zao hilo pamoja na maofisa mbalimbali kutoka katika Halmashauri ya Mbeya.

Malisa alisema kuna baadhi ya mawakala wananunua maua mabichi kwa wakulima ili kufikia malengo ambayo wanakuwa wamepangiwa na viongozi wa kampuni hizo.

Alisema mbinu hizo zinazofanywa na mawakala hao zinasababisha soko la zao hilo kuharibika na hata sifa za pareto inayozalishwa katika wilaya hiyo inaanza kuchafuliwa.

"Nyie ni wadau wetu tunaomba muwe wakali kwa mawakala hao ambao wanadanganya, kuna njia mbili za kukomesha tabia hiyo. Moja ni kuwachukulia hatua hao wanaodanganya ama kutoa motisha kwa wale wanaoleta iliyokidhi viwango," alisema Malisa.

Alisema Wilaya ya Mbeya ndiyo inaongoza kwa uzalishaji wa zao hilo nchini na kwamba pareto inayozalishwa kwenye wilaya hiyo ina ubora kuliko inayozalishwa kwenye maeneo mengine.

Malisa aliwataka mawakala ambao wanafanya udanganyifu kuacha mara moja ili kuepuka kuchukuliwa hatua za kisheria ikiwamo kupelekwa mahakamani. Aliwataka wakulima pia kuacha kuuza maua ambayo hayajakauka kwa maelezo kuwa wanachangia pia kuharibu soko la zao hilo ambalo limekuwa likiwaingizia kipato.

Baadhi ya wanunuzi wa zao hilo, waliomba serikali kusaidia kutoa elimu kwa wakulima wakidai kuwa wamekuwa wakiwaelimisha kuuza maua yao baada ya kukausha lakini bado hawatekelezi.

Mmoja wa wanunuzi hao, Gerald Joseph, alisema waliamua kuwasaidia wakulima kwa kuwajengea vikaushio maalumu ili wasihangaike lakini hawavitumii na badala yake wanauza pareto mbichi.

Alisema katika wilaya hiyo pekee wamejenga zaidi ya vikaushio 280 ambavyo walitoa elimu kwa wakulima namna ya kuvitumia lakini havitumiki ipasavyo.

"Ukipita huko kwa wakulima utakuta vikaushio vingi, lakini wengi hawavitumii wakidai kuwa vinawachelewesha, hivyo wanaamua kuuza maua mabichi," alisema Gerald.

Naye Mchungaji Obed Mwalenge aliomba viongozi wa serikali wapatiwe kwanza elimu juu ya kilimo cha zao hilo ili iwe rahisi kusimamia kwenye maeneo yao.

Alisema hata madiwani wanatakiwa kupatiwa elimu hiyo ili na wao wakaisambaze kwa wakulima katika maeneo wanayotokea badala ya kuziachia kampuni pekee.

Ofisa Kilimo wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Gideon Mapunda, alisema wamekuwa wakitoa elimu ya kilimo bora cha zao hilo, uchumaji na ukaushaji ili kuhakikisha ubora unabaki ule unaohitajika.

Alisema halmashauri imeanzisha utaratibu wa kutoa vibali maalumu kwa wanunuzi na wasafirishaji wa zao hilo ili kuondoa vishoka.



Mkuu wa Wilaya ya Kyela, Josephine Manase (wa tatu kushoto), akiwa na watendaji wa Shirika la Bima la Taifa wakishuka kwenye meli ya Mbeya II iliyofanyiwa matengenezo baada ya kupata hitilafu wakati inatia nanga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wananchi waondolewa hofu kuhusu homa ya nguruwe

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI imewatoa hofu wananchi kuwa ugonjwa wa homa ya nguruwe hauna madhara yoyote kwa binadamu kama ambavyo imekuwa ikielezwa na baadhi ya watu.

Kumekuwa na uvumi kuwa binadamu akila nyama ya nguruwe mwenye ugonjwa huo anaweza akadhurika, hatua iliyosababisha wengi kuogopa kula hasa katika kipindi ambacho kunakuwa na mlipuko huo.

Daktari wa Mifugo wa Mkoa wa Mbeya, Dk. Samora Mshang'a, aliyasema hayo juzi alipozungumza na Nipashe kuhusu hofu ambayo imekuwapo miongoni mwa wananchi wanaotumia kitoweo hicho.

Alisema ugonjwa huo ni hatari kwa nguruwe lakini hauna madhara yoyote kwa binadamu hata kama atakula nyama ya nguruwe mwenye ugonjwa.

"Nguruwe ambaye ameumwa ugonjwa huu anakufa ndani ya kipindi kifupi, hata kukonda hakondi na nyama yake ni nzuri na inaweza ikaliwa na binadamu pasipo kumdhuru kwa namna yoyote," alisema.

Dk. Mshang'a alisema ugonjwa wa homa ya nguruwe unaenezwa na virusi na hauna tiba na kwamba kinachowafanya wasisitize nguruwe aliyekufa na ugonjwa huo kutoliwa ni kwa sababu ya kuepuka kuendelea kusambaza homa hiyo.

Alisema usafirishaji wa nyama hiyo kutoka eneo moja kwenda lingine kunaweza kusababisha kuendelea kusambaa na kuathiri wanyama wengi zaidi.

Ili kudhibiti ugonjwa huo, alisema wafugaji wanapaswa kuwapa nguruwe chakula cha kutosha, kuzingatia usafi wa mabanda, kuhakikisha nguruwe wote wanafanyiwa ukaguzi wa kitaalamu pamoja na kuhakikisha nguruwe waliopata ugonjwa wanafukiwa kwenye shimo refu au wanachomwa moto.

"Kama nilivyosema awali ugonjwa huu hauna tiba hivyo kuchukua tahadhari za mapema ili kudhibiti usiingie ndio jambo la msingi na sisi kwenye mikoa yetu ya nyanda za juu kusini tulishaweka zuio la usafirishaji wa nguruwe muda mrefu hivyo wananchi wanapaswa kutopuuza hili agizo," alisema.

Aliongeza kuwa ugonjwa huo upo nchini kwa muda mrefu lakini huzuka kwa kasi zaidi kipindi cha masika kwa sababu uwezekano wa kusambaa kwa sababu ya maji kuwa mengi ni mkubwa.

Aliwataka wafugaji kuzingatia mbinu bora za ufugaji wanazoelekezwa na wataalamu wa mifugo huku akiwataka kutoa taarifa mapema kwa madaktari wa mifugo wanapoona dalili za ugonjwa huo.

# Mbunge akabidhi kitanda hospitalini

**Na Nebart Msokwa,** TUKUYU

MBUNGE wa Viti Maalumu Mkoa wa Mbeya, Suma Fyandomo, amekabidhi msaada wa kitanda cha kujifungulia na mashuka 30 kwa ajili ya wodi ya wanawake katika Hospitali ya Wilaya ya Rungwe ili kupunguza uhaba wa vifaa hivyo.

Alikabidhi vifaa hivyo kwa uongozi wa hospitali hiyo juzi ambapo aliahidi kuendelea kutoa msaada wa vifaa hivyo katika hospitali zingine za wilaya katika mkoa huo kwa awamu tofauti.

Alisema alitoa vifaa hivyo kwa lengo la kuiunga mkono serikali katika juhudi zake za uboreshaji wa huduma za afya kwa wananchi hususani huduma ya mama na mtoto.

Fyandomo alisema serikali imefanya kazi kubwa ya kuboresha huduma ya mama na mtoto katika hospitali hiyo lakini kuna baadhi ya matatizo madogo ambayo yamebakia na yanahitaji ushiriki wa wadau kuyatatua.

"Hiki kitanda nina uhakika kitawasaidia wanawake wenzangu wakati wa kujifungua, lakini leo nimefarijika sana maana wakati nakabidhi kitanda hiki na mashuka nimekutana na tukio la binti mmoja kujifungua mapacha watatu, na amejifungua vizuri.

"Nawapongeza madaktari wetu waliomsaidia binti huyu, naamini hata hivi vifaa nilivyovileta vitasaidia na vitatumika vizuri, niwaombe wataalamu muendelee na moyo huo wa kujitolea," alisema Fyandomo.

Akipokea vifaa hivyo, Kaimu Mganga Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Dk. Enock Mbikiwa, alimshukuru mbunge huyo kwa msaada huo na kwamba utasaidia kutatua kero ya wanawake wanaojifungua kusubiriana.

Alisema kwa siku wanajifungua wanawake wasiopungua 10 na hivyo wanatakiwa kuwa na vitanda vinavyoendana na idadi hiyo lakini kabla ya kupokea kitanda hicho walikuwa na vitanda saba pekee.

Dk. Mbikiwa alisema kutokana na hali hiyo baadhi ya wanawake walikuwa wanalazimika kusubiriana jambo ambalo alisema sio zuri kitaalamu.

"Tunashukuru kwa msaada huu tulioupokea, hospitali yetu inahitaji angalau vitanda 10 kwa ajili ya kujifungulia, sasa baada ya mbunge wetu kutusaidia tunahitaji vitanda vingine viwili ili sasa tuwe tumefikia mahitaji," alisema Dk. Mbikiwa.

Alisema serikali imejenga jengo la mama na mtoto katika hospitali hiyo ambalo ni la kisasa na linatosheleza mahitaji na kwamba wanaendelea na juhudi za kutafuta vifaa vyote muhimu kwa ajili ya mama na mtoto.



# Wanawake waitwa kupata msaada wa kisheria

**Na Mwandishi Wetu**

WANAWAKE wametakiwa kujitokeza kupata huduma za msaada wa kisheria katika kukabiliana na changamoto zinazowakabili katika jamii ikiwamo matatizo na mivutano katika ndoa.

Mkurugenzi wa Idara ya Msaada wa Kisheria, Hanifa Abdalla Said, aliyasema hayo jana wakati akizungumza na wananchi wakiwamo wasaidizi wa sheria katika wilaya za Unguja.

Alisema Serikali ya Zanzibar imeanzisha idara ya msaada wa kisheria kwa ajili ya kutoa huduma za changamoto zinazowakabili wanawake ambao wengi wao ni wanyonge ambao hawana uwezo wa kutafuta wawakilishi au wanasheria katika kusimamia mwenendo wa kesi zao.

Alisema utafiti mdogo unaonyesha kwamba asilimia 70 ya wananchi wanakabiliwa na changamoto za kupata msaada wa kisheria katika matatizo mbalimbali yanayowakabili ikiwamo mivutano katika ndoa.

Alisema wananchi wengi bado hawana uelewa wa masuala ya kisheria zaidi waliopo vijijini ambapo hujitokeza matukio ya kudhulumiana ardhi na masuala ya kifamilia.

"Hizo ndiyo sababu za kuundwa kwa idara ya msaada wa huduma za kisheria ili kutoa huduma kwa makundi ya wananchi wanyonge ambao hawana uwezo wa kisheria katika kupata huduma hizo," alisema.

Hanifa alisema wamejipanga zaidi kushuka hadi katika wilaya zote za Unguja na Pemba katika kufikisha huduma za kisheria kwa wananchi.

Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Mansura Mossi Kassim, alisema wizara imejipanga kikamilifu kuona malengo yaliyowekwa na serikali katika idara ya msaada wa huduma za kisheria yanafikiwa kikamilifu.

Alisema tayari wamefanya mawasiliano na viongozi wa mikoa pamoja na wakuu wa wilaya kuona njia zitakazotumika katika kuona wananchi wanafikiwa na huduma za msaada wa kisheria katika kila kona.

Alisema bado huduma hizo hazijafika vizuri vijijini ambapo hivi sasa kumejitokeza matukio ya wananchi kuhitaji msaada wa kisheria katika kukabiliana na matukio mbalimbali ikiwamo mivutano ya kesi za ardhi.

# Mapagale ya nyumba yatajwa sehemu kuu matukio ya ukatili dhidi ya watoto

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MATUKIO ya ukatili na udhalilishaji dhidi ya watoto visiwani Zanzibar yametajwa kutokea zaidi nyakati za usiku na hutendeka hasa kwenye mapagale.

Kwa mujibu wa taarifa ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar, Sabina Raphael Daima, ambaye ni Mkuu wa Vidisheni ya Jinsia na Ajira, matukio yaliyoripotiwa Juni, mwaka huu yalikuwa 127 na kati ya hayo 80 ni ya ubakaji ambayo ndiyo yanaongoza.

Daima alisema katika matukio hayo yaliyoripotiwa, matukio 48 yamefanyika katika nyumba mbovu, 13 yamefanyika katika nyumba za kulala wageni, 27 nyumbani kwa watuhumiwa na 26 porini.

Alisema waathirika wa matukio hayo ni 128 ambapo kati yao, watoto ni 110 sawa na asilimia 85.9, wanawake 13 sawa na asilimia 10.2 na wanaume watano sawa na asilimia 3.9.

"Matukio ya kubaka ni 80, kulawiti na kunajisi 22, kutorosha tisa, shambulio la aibu na kukashifu manane na shambulio ni matukio manane," alisema Daima.

Kiongozi huyo alisema idadi ya matukio hayo kwa mwezi wa Juni yamepungua kwa asilimia 17.5 kutoka matukio 154 kwa mwezi wa Mei mwaka huu hadi matukio 127 Juni.

Hata hivyo, alisema matukio ya kubaka, kulawiti na kutorosha yameripotiwa kuongezeka kwa mwezi wa Juni. Alisema Wilaya ya Mjini Unguja imeripotiwa kuwa na matukio mengi ambapo ni 25 ikifuatiwa na Wilaya ya Magharibi B, Unguja.

Alisema Wilaya ya Kusini Unguja imeripotiwa kuwa na idadi ndogo ya matukio kuliko wilaya zote za Zanzibar ambayo ilikuwa na matukio mawili pekee kwa mwezi huo.

"Katika matukio 80 ya ubakaji yaliyoripotiwa kwa mwezi wa Juni, tisa waathirika wake ni wanawake, wasichana ni 71, wavulana waliolawitiwa ni 22," alisema.

Alisema matukio 106 kati ya 127, yameripotiwa yapo chini ya upelelezi wa Jeshi la Polisi sawa na asilimia 83.5, matukio 16 yapo mahakamani sawa na asilimia 12.6 na matukio matano yamefungwa polisi sawa na asilimia 3.9.



Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Zanzibar (SUZA), Dk. Salim Suleiman Ali, akizungumza na wanawake wanaotarajia kushika nafasi za uongozi kupitia vyama mbalimbali vya siasa wakati akiwasilisha mada ya mwongozo wa sera ya jinsia kwenye mafunzo ya kuwajengea uwezo yaliyoandaliwa na Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Zanzibar (TAMWA), kupitia mradi wa kuwainua wanawake kushika nafasi za uongozi (SWIL) Tunguu, Wilaya ya Kati Mkoa wa Kusini Unguja jana. **PICHA: MAELEZO**

# PBZ mdhamini mkuu tamasha la Kizimkazi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KATIKA kuelekea tamasha la Kizimkazi Festival mwaka 2023, Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) imejitokeza kuwa wadhamini wakuu wa tamasha hilo ambalo hufanyika Agosti ya kila mwaka.

Tamasha hilo hujumuisha shughuli mbalimbali za kijamii ikiwamo ujenzi wa miradi ya maendeleo, michezo na kudumisha mila na tamaduni.

Akizungumza katika hafla ya makabidhiano ya vifaa vya michezo vilivyotolewa na benki hiyo yaliyofanyika katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja Tunguu, Mkurugenzi wa Biashara wa Benki hiyo, Eddie Mhina, alisema kwa mwaka huu, wameamua kuwa wadhamini wakuu.

Alisema vifaa hivyo vitasaidia katika kuibua vipaji vya vijana wa kijiji hicho ili kukuza taaluma ya michezo mbalimbali ambayo itafanyika katika tamasha hilo.

Alisema licha ya kutoa vifaa hivyo, benki hiyo itakuwa na shughuli mbalimbali za kimaendeleo siku hiyo ikiwa ni pamoja na miradi ya kuboresha majengo ya shule yaliochakaa ikiwamo Shule ya Muyuni ili kuwezesha wanafunzi kupata elimu katika mazingira mazuri.

Akizungumzia lengo la kudhamini tamasha hilo, alisema litaleta fursa za utalii, kiuchumi na michezo, hivyo PBZ kwa kutambua fursa hizo imeunga mkono serikali katika kuinua uchumi kupitia sekta hizo na kuboresha afya kupitia michezo.

Mkurugenzi wa Masoko wa PBZ, Seif Mohamed, alisema lengo la udhamini wa vifaa hivyo ni kuunga mkono jitihada za serikali za kuinua michezo.

Alisema PBZ ina wajibu wa kushirikiana na jamii katika masuala mbalimbali ikiwamo ya kijamii na kiuchumi.

Mwenyekiti wa Kamati ya Udhamini wa Mashindano ya Kizimkazi Festival, Mpate Abdallah na Katibu wa Kamati Kuu Mtendaji ya mashindano hayo, Hamid Abdul-hamid Khamis, waliipongeza PBZ kwa kuwapa vifaa hivyo ambavyo vitasaidia kuanza mashindano hayo kwa wakati.

Waliwaomba wananchi wa Zanzibar kushiriki katika tamasha hilo ambalo litawawezesha kuona na kujifunza mambo mbalimbali muhimu.

Tamasha hilo ambalo kilele chake kitakuwa Agosti 30, mwaka huu, mgeni rasmi anatarajia kuwa Rais Samia Suluhu Hassan.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI**
**IDARA YA UHAMIAJI**



**OMBI LA URAIA LA NDUGU PRASHANT DETHA**
Mwenye picha hapo juu, anaomba uraia wa Tanzania kwa Mh. Waziri wa Mambo ya Ndani ya nchi, utaifa wake kwa sasa ni INDIAN nchi atokayo INDIA shughuli zake ni **MFANYA BIASHARA anwani ZINGA KWA MTORO (BAGAMOYO)** yupo nchini tangu 2004.

Kwa yeyote mwenye taarifa/sababu za kwanini mwombaji asipewe uraia wa Tanzania, atume taarifa ya maandishi kwa Kamishna Jenerali wa Uhamiaji, S.L.P 512 Dar es salaam.
KUMB. NA. DN 572917.

INSP. MAGRAM A. BAJHANUN
UHAMIAJI WILAYA
BAGAMOYO

## KUPOTEA KWA VYETI



MEBO EZEKIEL KANYABUHA anatangaza kupotea kwa cheti cha Diploma in Community Development chenye namba RU/DCD/V/679 kilichotolewa na Rungemba CDTI mwaka 2013. Cheti cha Degree in Community Development chenye namba TBD16 – 142 kilichotolewa na Tengeru Institute of Community Development mwaka 2016. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: CHD/RB/1198/2023 au apige simu namba 0628 823 572.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya.........TANGA**
**Kituo cha MJINI TANGA......Mkoa...TANGA**
**Usimamizi wa Mirathi Na......128/2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU: FAUZY KHALID ABDALLAH**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI**
**YALIYOLETWA NA: MOHAMED FAUZY KHALID**

**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo tarehe 27 Mwezi 7 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Zingatia;
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
*Marehemu hakuacha wosia
ImetolewaleoTarehe ....20... mwezi ...7...mwaka 2023

HAKIMU

## KUPOTEA KWA PASSPORT



ALLY JUMA MAZOLA anatangaza kupotea kwa hati yake ya kusafiria (Passport) yenye namba TAE 283075 iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Dar es salaam tarehe 17/01/2020. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: DAR/URA/RB/238192/2023.

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

SHAMIM DAUD anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba ya usajili T 485 ABR – TOYOTA HILUX. Chassis namba YN1070002503. Engine namba 3Y1279259. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: ARU/ARU/RB/242015/2023.

**INTHEDISTRICTCOURTOFDODOMA**
**ATDODOMA**
**Probate and Administration Cause No.75 of 2023**
**In the matter of the Estate of the late**
**ZAWADI FILIMONI MWAPONGO**
**of KIKUYU MISSION within Dodoma Region**
**And**
**In the matter of the application for letters of administration by**
**MERKIZEDE KISAMSON MANGASIN**

**GENERAL CITATION**
**( Rule 75 of Probate Rules Gn.369 of 163 )**

AllPERSONS claiming to have any interest in the Estate of the above named decease dare hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before thegrant ofl etters of Administrations made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 24 Day of 7,2023

Date at Dodoma this 27 day of 6, 2023.

RESIDENT MAGISTRATE

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

ELIA MAGHEE NYEURA anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba ya usajili T 678 DEJ – TOYOTA IST. Chassis namba NCP650015441. Engine namba 1NZ14276. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: ARU/ARU/RB/226573/2023.

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

JUMANNE SUMARA SIMAMA anatangaza kupotea kwa kadi ya Pikipiki yenye namba ya usajili MC 313 DVQ – TVS HLX 125. Chassis namba MD62SAF44P1A05986. Engine namba DF4AP1005957. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: DAR/CEN/RB/237679/2023.

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

BAKARI SHARIFU BAKARI anatangaza kupotea kwa kadi ya Pikipiki yenye namba ya usajili MC 767 DUD – BOXER BM 125. Chassis namba MD2B15BX4PWL85304. Engine namba JVXWPL51301. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: DAR/CEN/RB/237272/2023

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

DENSIANA SIMON MBABILANYA anatangaza kupotea kwa kadi ya Pikipiki yenye namba ya usajili MC 833 DSG – BOXER BM 125. Chassis namba MD2B15BX8NWH9183. Engine namba JVXWNH41953. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: DAR/CEN/RB/234835/2023.

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

WILFRED SAYOLOI MOLLE anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba ya usajili T 795 CML – TOYOTA HILUX. Chassis namba JTFDS696300039033. Engine namba 2KD1196800. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: ARU/ARU/RB/244683/2023.

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

BERTHA CHRISTOSIA KOKA anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba ya usajili T 262 AMG – TOYOTA RAV 4. Chassis namba SXA100052710. Engine namba 3S1822471. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: ARU/ARU/RB/244646/2023.

*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Piga Simu 0677020701*

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.
MOB: +255 - 0677020701
E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ,
WEBSITE: WWW.IPPMEDIA.COM**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.




Kaimu Ofisa Uhusiano wa Chuo cha Usafirishaji (NIT), Juma Manday, akitoa malekezo kwa wananchi waliotembelea banda la chuo hicho, kujua utendaji kazi wake katika Maonyesho ya 18 ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia (TCU), Viwanja vya Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Ujenzi vituo gesi asilia kwa ajili ya magari waiva TPDC

**Na Restuta James**

SHIRIKA la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), liko katika hatua za mwisho kuanza ujenzi wa kituo kikuu cha kujaza gesi asilia kwenye magari na kwa matumizi ya nyumbani ili kurahisisha upatikanaji wa nishati hiyo.

Lengo la kuwapo kwa huduma hizo ni kuhamasisha matumizi ya gesi kwenye vyombo vya usafiri kama daladala, bajaji, bodaboda, mabasi na malori badala ya kutumia dizeli na petroli. Hatua hiyo pia inalenga kupunguza uharibifu wa mazingira.

Akizungumza na wahariri wa vyombo mbalimbali vya habari jijini Dar es Salaam jana, Mkurugenzi Mtendaji wa TPDC, Mussa Mohamed Makame, alisema kituo kikuu kitajengwa eneo la Mlimani City na vidogo viwili vitajengwa Muhimbili na Kibaha.

"Tunategemea ujenzi wake utafanyika ndani ya miezi minane. Tumezungumza na Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini (GPSA) ili tujenge vituo barabara kuu ya Morogoro hadi Dodoma, kwa ajili ya kujaza magari ya serikali. Tumeita sekta binafsi na zipo kampuni ambazo zimeonyesha nia ya kuongeza vituo vya gesi asilia kwenye vituo vyao vya mafuta," alisema.

Makame alisema katika kutekeleza hilo, wataugawa mkoa wa Dar es Salaam kanda kwa kanda ili iwe rahisi na kuhakikisha kila upande unajengwa vituo hivyo.

"Tutaangalia kila barabara kuu na kama nilivyosema kwa kuanzia tutaanza na barabara ya Morogoro kuanzia Dar es Salaam hadi Dodoma. Tutaenda Kaskazini, Nyanda za Juu Kaskazini na Kusini. Nia ni kuhamasisha matumizi ya gesi, lakini pia kusogeza huduma karibu na wananchi," alisema.

Makame alisema baadhi ya kampuni zinazomiliki vituo vya mafuta zimeonyesha nia ya kuongeza sehemu ya kujaza gesi asilia kwenye magari.

Mkurugenzi wa Mipango na Uwekezaji wa TPDC, Derick Moshi, alisema mkakati ni kuuza gesi hiyo katika nchi za Afrika Mashariki kama Kenya na Uganda na Kusini mwa Tanzania.

Alisema TPDC inatarajia pia kujenga maghala makubwa ya kuhifadhi mafuta ili Tanzania iwe kituo kikuu cha mafuta kwa ajili ya kuhudumia nchi zisizo na bandari.

Pia alisema TPDC inakusudia kuongeza mtandao wa usambazaji wa gesi asilia kwa njia ya mabomba na gesi iliyoshindiliwa (CNG), kuendelea kushiriki kwa ufanisi katika biashara ya kuagiza mafuta kupitia mfumo wa uagizaji wa pamoja na kuhakikisha mitambo ya kuchakata na kusafirisha gesi inafanya kazi kwa asilimia 100.

Mkurugenzi wa Fedha na Utawala, Francis Mwakapalila, alisema mwaka wa fedha uliopita, TPDC ililipa Sh. bilioni 62.84 kwenye mfuko wa usimamizi wa mafuta na gesi, kodi ya Sh. bilioni 57.5, gawio la Sh. bilioni 2.7 na kupata faida ya Sh. bilioni 97.78.

Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), Deodatus Balile, aliyashauri mashirika na taasisi za serikali kutoa taarifa za mara kwa mara kwa umma kuhusu miradi inayofanywa ili wananchi wajue fursa zilizopo.

# Uholanzi yaiahidi ushirikiano Tanzania kijamii na kiuchumi

**Na Benny Mwaipaja,**
NEW YORK



UHOLANZI imeahidi kuendeleza ushirikiano na Tanzania katika nyanja mbalimbali za kiuchumi na kijamii, ikiwamo utekelezaji wa miradi ya kimkakati itakayochangia kukuza maendeleo ya nchi na watu wake.

Ahadi hiyo ilitolewa jana jijini hapa na Naibu Waziri wa Mambo ya Ushirikiano wa Kimataifa wa Uholanzi, Steven Collet, alipokutana na kufanya mazungumzo na Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha, Dk. Natu Mwamba, kando ya Mikutano ya Jukwaa la Juu la Siasa ya Umoja wa Mataifa inayojadili tathmini na utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030.

Aidha, aliahidi kuwa serikali yake itaongeza ufadhili kwenye miradi mbalimbali ikiwamo ya kilimo, nishati, uongezaji thamani wa madini, kusaidia wajasiriamali wadogo pamoja na ujenzi wa baadhi ya miundombinu inayotekelezwa na Tanzania.

Naye Dk. Mwamba, ambaye ni Mlipaji Mkuu wa Serikali, alishukuru Uholanzi kwa ushirikiano wa kimaendeleo inayotoa kwa Tanzania ikiwamo kusaidia utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kupitia Umoja wa Ulaya (EU).

Alisema Tanzania ina mengi iliyonufaika kutoka Uholanzi ikiwamo ufadhili wa miradi ya kilimo, afya, elimu na mingine kadha wa kadha inayotekelezwa na sekta binafsi na kwamba ushirikiano huo utaendelea kuzinufaisha pande zote mbili.

Aidha, aliiomba Uholanzi kuisaidia Tanzania kufikia masoko ya fedha kwa ajili ya kusaidia kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi kwa njia ya kuuza hewa ukaa, ambayo ni biashara kubwa duniani hivi sasa na kwamba Tanzania ina sifa za kunufaika na mpango huo kwa kuwa ina rasilimali nyingi zinazotakiwa kuhifadhiwa na kuingizia nchi fedha za kigeni.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470DODOMA,
20.07.2023

## TAARIFA KWA UMMA

1. Ndugu Wananchi mnatangaziwa kua siku ya tarehe **25.07.2023** hadi **07.08.2023** kampuni ya **CEVA Interfreight** itasafirisha gari tupu wenye vipimo vikubwa kutoka **Bandari ya Dar Es Salaam** kuelekea **Mzenga**, gari hilo lenye namba za usajili

**NRB97300 / NRB15200 / DS00TG GP / NRB43293**

2. Gari hizo zina vipimo vifuatavyo:

**Urefu - mita 36.0 Upana - mita 7.5 Kimo - mita 4.6**

3. Njia itakayotumika: **Bandari ya Dar Es Salaam** hadi **Mzenga** kupitia **Barabara ya Mandela, Barabara ya Morogoro** mpaka **Mlandizi**, magari yatasafiri muda wa usiku ( **Kuanzia saa 08:00 Usiku mpaka saa 11:00 Alfajiri**). Kutoka **Mlandizi** kwenda **Mzenga** magari yatasafiri muda wa mchana ( **Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni**).

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza**

## ARM SOLUTION AUCTION MART AND PROPERTY MANAGEMENT CO LTD

KWA IDHINI TULIYOPEWA NA MUCOBA Bank Plc TUNAWATANGAZIA WANANCHI WOTE KUWA KUANZIA TAREHE 07-08-2023 NA KUENDELEA TUTAUZA KWA MNADA WA HADHARA MALI ZA WADAIWA HAPO CHINI ILI KUFIDIA MADENI WANAYODAIWA.

| NO | JINA LA MDAIWA | TAWI ALILOKOPA | DHAMANA | MAHALI ILIPO | TAREHE YA MNADA/ MUDA |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | LEONARD RAPHAEL MGINA | IRINGA | NYUMBA PLOT NO. 160 BLOCK "B" | KATA YA MTWIVILA - IRINGA | NA KUENDELEA KUANZA SAA 03 ASUBUHI |
| 2. | STANLEY KIBITALE | MAFINGA | NYUMBA | MTAA WA IHONGOLE – MAFINGA | NA KUENDELEA KUANZA SAA 03 ASUBUHI |
| 3. | KIDUKO CHARLES MAIKO | MAFINGA | NYUMBA | KIJIJI CHA IGOWOLE-MUFINDI | NA KUENDELEA KUANZA SAA 03 ASUBUHI |
| 4. | MATHEW LWIDIKO CHAVALA | MAFINGA | NYUMBA | KIJIJI CHA IGOWOLE-MUFINDI | NA KUENDELEA KUANZA SAA 03 ASUBUHI |
| 5. | JOCTAN NYALUKE | MAFINGA | NYUMBA | MTAA WA IHONGOLE-MAFINGA | NA KUENDELEA KUANZA SAA 03 ASUBUHI |
| 6. | HENRY IBRAHIM LWEHELA | MAFINGA | NYUMBA | KIJIJI CHA IGOWOLE-MUFINDI | NA KUENDELEA KUANZA SAA 03 ASUBUHI |
| 7. | ANJELO ANDREAS NYEMBEKE | MAFINGA | NYUMBA MBILI, KIWANJA NO. 748 KITALU 'D' | MITAA YA IVAMBINUNGU NA NDOLEZI MAFINGA MJINI | NA KUENDELEA KUANZA SAA 03 ASUBUHI |

**MASHARTI YA MNADA**

MSHINDI ATATAKIWA KULIPA ASILIMIA (25%) AU ZAIDI BAADA YA NYUNDO YA DALALI NA BAKI (75%) ITALIPWA NDANI YA SIKU KUMI NA NNE (14), TOFAUTI NA HAPO MSHINDI ATAPOTEZA HAKI ZAKE NA MNADA UTARUDIWA UPYA.

**MAWASILIANO: 0757 -107 715, 0784 -759 892**

# TANZANIA BARA, BURUNDI KUFUNGUA CECAFA U-18

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU ya Soka ya Wasichana ya Tanzania Bara ya umri chini ya miaka 18 ya Tanzania itakutana na yosso wenzao wa Burundi katika mechi ya ufunguzi ya mashindano ya Afrika Mashariki na Kati (CECAFA U-18) itakayofanyika Julai 25, mwaka huu kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

Kwa mujibu wa ratiba iliyotolewa na Baraza la Soka la Nchi za Afrika Mashariki na Kati (CECAFA), mechi nyingine za ufunguzi zitakuwa ni kati ya Zanzibar dhidi ya Rwanda wakati Ethiopia watavaana na Uganda.

Tanzania Bara itashuka tena dimbani Julai 28, mwaka huu kuvaana na Ethiopia na siku tatu baadaye itakutana na 'ndugu' Zanzibar.

Michuano hiyo inayoshirikisha nchi sita na itakayochezwa kwa mkondo mmoja itamalizika Agosti 6, mwaka huu.

Wakati huo huo, kikosi cha Zanzibar kimeingia kambini jana kwa ajili ya kujiandaa na mashindano hayo ambayo awali yalipangwa kufanyika Kenya.

Katibu wa Kamati ya Soka la Wanawake Zanzibar ambaye ni Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Khatma Mwalim, alisema wachezaji wake wanafanya mazoezi kwenye Uwanja wa Mao ze Dong na anaamini watafanya vyema kutokana na mazoezi waliyofanya.

"Tunatarajia kuendelea na mazoezi pale tulipoishia, kambi hii itakuwa ya muda mfupi kwa sababu tutakuwa tunajiandaa na safari ya kuelekea katika mashindano," alisema kocha huyo.

Aliongeza wachezaji wote walioitwa katika timu hiyo wanaotoka Unguja wako katika hali nzuri na wenzao kutoka Pemba wanatarajiwa kuwasili leo.

"Timu yetu kamili ina wachezaji 21, tumeshaanza mazoezi na wachezaji 15 huku wengine kutoka Pemba na maeneo mengine watajiunga na wenzao wakati wowote baada ya kuwaombea ruhusa katika klabu zao," Mwalim alisema.

Nchi wanachama wa CECAFA ambazo hazitashiriki mashindano hayo ni pamoja na Kenya, Sudan, Sudan Kusini, Djibouti, Eritrea na Somalia.



Mabeki wa Raha Queens ya Simiyu (jezi ya kijani), wakipambana kumzuia straika wa Ziba Sekondari ya Tabora katika mechi ya Ligi ya Mabingwa wa Mikoa ya Wanawake iliyochezwa kwenye Uwanja wa Nyamagana jijini Mwanza jana. Ziba ilipata ushindi wa mabao 10-0. **PICHA: TFF**

# Namungo, Singida FG kupimana

**Na Shufaa Lyimo**

KATIKA kukiimarisha kikosi chake, kikosi cha Namungo FC kinatarajia kucheza mechi ya kirafiki dhidi ya Singida Fountain Gate itakayofanyika Jumatatu kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini, Arusha imeelezwa.

Akizungumza na gazeti la Nipashe kutoka Karatu jana, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Denis Kitambi, alisema lengo la mchezo huo ni kuangalia uwezo wa kila mchezaji baada ya kuanza maandalizi ya msimu mpya unaotarajiwa kuanza ifikapo Agosti 15, mwaka huu.

Kitambi alisema anaamini mechi hiyo itaanza kumpa mwanga wa kikosi chake wakati bado dirisha la usajili likiwa halijafungwa.

"Tutacheza mchezo wa kirafiki wa kwanza Julai 24, mwaka huu na lengo ni kuangalia wachezaji wapya pamoja na wale wa zamani, tunahitaji kuona mapungufu na ubora wa kila mchezaji," alisema Kitambi.

Kocha huyo alisema mchezo huo pia utasaidia kuwaweka sawa wachezaji wake ambao wametoka katika mapumziko na kuanza kujiweka tayari kukabiliana na ushindani wa msimu mpya.

"Naweza kusema mpaka sasa tayari tumemaliza kufanya usajili, wachezaji wote wapo kambini hapa Karatu na kwa wale wapya tutawatangaza muda wowote kuanzia sasa. Tutafanya hivyo ili mashabiki wetu wafahamu kinachoendelea ndani ya kikosi chao," Kitambi alisema.

Aliongeza malengo ya timu yao katika msimu mpya ni kumaliza kwenye nafasi ya juu kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

## Mfungaji Bora U20 asajiliwa Mashujaa

**Na Adam Fungamwango**

KINARA wa mabao katika Ligi ya Vijana wa umri chini ya miaka 20, Athumani Masumbuko 'Makambo' amesajiliwa rasmi na Mashujaa FC ya Kigoma ambayo itashiriki Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao.

Makambo kutoka Mtibwa Sugar aliibuka Mfungaji Bora wa ligi ya vijana, akifunga mabao saba na kumwacha mpinzani wake, straika wa Azam FC, Cyprian Kichwele, aliyemaliza ligi hiyo akizifumania nyavu mara sita.

"Ninayo furaha kubwa kurudi kwenye klabu ya nyumbani Kigoma, nawaahidi mashabiki watapata furaha, nitaipambania timu hii ili ifanye vizuri katika kila mchezo," alisema mchezaji huyo baada ya kutambulishwa na klabu yake mpya.

Mchezaji hiyo aliipa ubingwa Mtibwa Sugar kwa kufunga bao pekee dhidi ya Geita Gold FC katika mechi ya fainali iliyochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

Mashujaa FC kutoka Ligi ya Championship ilipanda daraja baada ya kuifunga Mbeya City mabao 4-1 katika mechi za 'play off' imeweka kambi yake Zanzibar.

## Wasanii kusindikiza kampeni ya sheria

**Na Sabato Kasika**

VIKUNDI mbalimbali vya ngoma, sarakasi na ngonjera vinatarajiwa kupamba kampeni ya kitaifa ya Mama Samia Legal Aid Campaign itakayofanyika kuanzia kesho mkoani, Ruvuma.

Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Damas Ndumbaro, alisema hayo wakati akizungumza katika warsha inayohusu ukatili wa kijinsia kwa vyombo vya habari jijini, Dar es Salaam juzi.

Ndumbaro alisema kampeni hiyo ilianza mapema mwaka huu na imeshafanyika katika mikoa ya Manyara, Dodoma na Shinyanga, huku akifafanua sasa ni zamu ya Ruvuma.

Aliongeza lengo la kutumia vikundi hivyo ni kutaka kufikisha ujumbe kwa jamii, kupitia kampeni hiyo ni ya miaka mitatu na itaongeza kasi ya kutoa msaada wa kisheria na uelewa wa haki na wajibu.

"Pamoja na kazi nzuri inayofanywa na watoa huduma ya msaada wa kisheria, bado jamii yetu inakabiliwa na vikwazo kadhaa vinavyofifisha juhudi za serikali katika kufikia malengo tarajiwa," Ndumbaro alisema.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### CAICEDO, CHELSEA HAJASOMEKA
CHELSEA inafanyia kazi ofa iliyoboreshwa ya pauni milioni 80 pamoja na nyongeza kwa kiungo wa Brighton na Timu ya Taifa ya Ecuador, Moises Caicedo, mwenye umri wa miaka 21. **(Mail)**

### GUEHI KUREJEA CHELSEA
CHELSEA pia inafikiria kumrejesha Marc Guehi, ikiwa imepita miaka miwili baada ya kumuuza beki huyo wa England mwenye umri wa miaka 23 kwa Crystal Palace. **(Guardian)**

### RAPHINHA KUMRITHI MAHREZ
MANCHESTER City inamtaka winga wa Barcelona ambaye ni raia wa Brazil, Raphinha mwenye umri wa miaka 26 ili kuchukua nafasi ya winga wao anayekwenda Al-Ahli, nyota wa Algeria, Riyad Mahrez (32). **(Foot Mercato)**

### MAXIMIN KUTUA SAUDIA
KLABU ya Newcastle United inakaribia kumuuza winga Mfaransa, Allan Saint-Maximin, mwenye umri wa miaka 26 kwa klabu ya Saudi Arabia, Al-Ahli kwa takriban pauni milioni 30. **(Telegraph)**

### AL NASSR, VILLA VITANI
KLABU ya Al-Nassr imeboresha dau lao la kumnunua, Moussa Diaby wa Bayer Leverkusen, huku Aston Villa wakiwasilisha ombi la pili kwa winga huyo wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 24. **(Fabrizio Romano)**

### DAU LA DOUCOURE LATAJWA
KLABU ya Crystal Palace inatarajiwa kuweka thamani ya kima cha chini cha pauni milioni 70 kwa kiungo wa kati wa Mali, Cheick Doucoure, mwenye umri wa miaka 23, ambaye anawindwa na Liverpool. **(Mail)**

### PEDRO ATAKIWA SPURS
TOTTENHAM Hotspur inafikiria kumnunua mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Brazil, Pedro, mwenye umri wa miaka 26 anayechezea Flamengo. **(Independent)**

### FRESNEDA AGOMBEWA ULAYA
DAU la pauni milioni 15 linaweza kutosha kwa Bournemouth kuzishinda klabu za Borussia Dortmund, Barcelona na Real Madrid katika usajili wa beki wa Hispania, Ivan Fresneda, mwenye umri wa miaka 18 kutoka Real Valladolid msimu huu. **(Football Insider)**

### FULHAM YAMTAKA BASSEY
FULHAM imetoa ofa ya awali ya pauni milioni 15 kwa Ajax ili kumnunua beki wa Timu ya Taifa ya Nigeria, Calvin Bassey, mwenye umri wa miaka 23. **(Athletic)**

### FELIX AKARIBIA BARCELONA
KLABU ya Atletico Madrid imempa mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Ureno, Joao Felix, mwenye umri wa miaka 23 idhini ya kukamilisha uhamisho wake wa kujiunga na Barcelona. **(AS)**

### VERRATTI ANUKIA ATLETICO
ATLETICO Madrid imewasiliana na Paris St-Germain kuhusu upatikanaji wa Marco Verratti, lakini bado hawajatuma ofa kwa kiungo huyo wa kati wa Timu ya Taifa ya Italia mwenye umri wa miaka 30. **(L'Equipe)**

### CHELSEA YAMFUATA WAHI
CHELSEA huenda ikakamilisha uhamisho wa Elye Wahi wa Montpellier, lakini Atletico Madrid pia inamwania mshambuliaji huyo wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 20. **(L'Equipe)**

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# ROONEY AMTABIRIA MAKUBWA RICE EPL

Asema anaamini kiungo huyo atakuwa 'mchezaji kiongozi' wa Arsenal katika...

**WASHINGTON, Marekani**

GWIJI wa soka wa England, Wayne Rooney, anaamini, Declan Rice atathibitisha "mchezaji mkubwa" na kiongozi muhimu kwa Arsenal, wakati wakijaribu kuwania taji la Ligi Kuu England katika msimu mpya, kwa mujibu wa PA.

Kiungo huyo mwenye umri wa miaka 24 alikamilisha uhamisho wake wa pauni milioni 105 kutoka West Ham hadi kutua kwenye Uwanja wa Emirates wikiendi iliyopita, akisaini mkataba wa muda mrefu na klabu hiyo ya Kaskazini ya jiji la London.

Mara moja Rice aliondoka na wachezaji wenzake wapya hadi Washington DC, ambapo Arsenal walianza ziara yao ya kujiandaa na msimu mpya huko Marekani dhidi ya nyota wa Ligi Kuu ya nchi hiyo (MLS), juzi na walishinda mabao 5-0.

Kocha Mkuu wa DC United, Rooney ndiye aliyekuwa akiwaongoza nyota wenyeji na anaamini vijana wa Mikel Arteta wamepata sifa muhimu wanapotazamia kushinda taji la Ligi Kuu England la msimu huu mpya.

"Nadhani anaweza kuwa ndiye anayeweza ... vizuri, lazima awe kiongozi sasa, kwa kweli, nadhani timu ya Arsenal ilikuwa inamhitaji mtu kama yeye," alisema Rooney akiliambia Shirika la Habari la PA.

"Nilimwona Frank Lampard akisema anahisi Declan anaweza kuwa nahodha wa Chelsea kwa miaka 10 ijayo ikiwa angeenda huko.

"Nadhani anaweza kufanya hivyo (kwa Arsenal) na anaonekana kuwa na tabia hiyo na ninaamini atakuwa mchezaji mkubwa wa Arsenal."

Rooney anajua jambo moja au mawili kuhusu matarajio yake baada ya uhamisho wa fedha nyingi, kwani yeye alistawi baada ya kujiunga na Manchester United kutoka Everton mwaka 2004.

Rooney mwenye umri wa miaka 37 anatarajia hivyo hivyo kutoka kwa Rice na kiungo mwenzake wa kati wa England, Jude Bellingham, ambaye mwezi uliopita alikamilisha uhamisho wa kujiunga na Real Madrid kwa dau la awali la pauni milioni 88.5 na kupanda hadi kufikia pauni milioni 115.

# BAYERN MUNICH KUTOMUUZA KIMMICH




**MUNICH, Ujerumani**

BAYERN Munich imeweka wazi msimamo wao kuhusu kiungo wa kati, Joshua Kimmich, haujabadilika na hawana nia ya kumwacha aondoke katika klabu hiyo msimu huu wa joto, kwa mujibu wa 90mins.

Hatima ya kiungo huyo wa kati wa Ujerumani imeangaziwa baada ya kuibua wasiwasi kuhusu mahali anapojiona kwa muda mrefu na ikiwa hiyo inamaanisha atabaki Bayern.

Habari za uwezekano wa Kimmich kutokuwa shwari pale kwenye Uwanja wa Allianz Arena hazikuonekana kote Ulaya. Inaaminika Arsenal, Chelsea, Liverpool, Manchester City na Manchester United wote walikuwa wakifahamishwa kuhusu hali yake, pamoja na Barcelona na Paris Saint-Germain.

Barcelona na Manchester City waliibuka ndio wanaotarajiwa kuwa na uwezekano mkubwa wa kuwasilisha ofa zao msimu huu, lakini Bayern Munich walijibu kwa kusisitiza hawana mpango wa kumuuza.

Wiki hii Kocha Mkuu, Thomas Tuchel aliulizwa kuhusu hali yake na alikiri lolote linawezekana katika soka.

"Itashangaza. Lakini dirisha la uhamisho ni dirisha la uhamisho, nilisema kwa ujumla lolote linawezekana.

"Hakuna maana kabisa kuangusha jina na kurusha jina tofauti kila siku," alisema bosi huyo wa Bayern, ambaye amesisitiza Kimmich bado ni sehemu muhimu ya mipango yake.

Kimmich bado yuko chini ya mkataba pale hadi msimu wa joto wa mwaka 2025.

# Aubameyang akaribia kutua Marseille



**MARSEILLE, Ufaransa**

PIERRE-Emerick Aubameyang amemaliza muda wake na Chelsea na anajiunga na Marseille kwa uhamisho huru, vyanzo vimeiambia ESPN.

Aubameyang anakaribia kukubali mkataba wa miaka mitatu kujiunga na miamba hao wa Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1.

Mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 34 alikuwa na wakati mgumu wa kupata namba katika kikosi cha Chelsea, ambapo alicheza mechi 21 baada ya kujiunga nayo Septemba mwaka jana huku akifunga mabao matatu pekee.

Uhamisho huo utaashiria kurejea kwake Ligue 1 baada ya miaka 10 kufuatia kukaa Saint-Etienne kati ya mwaka 2011 na 2013.

Chelsea wamekumbwa na misukosuko katika kikosi msimu huu, pamoja na kuwasili kwa kocha mpya, Mauricio Pochettino.

Kocha huyo raia wa Argentina aliiambia ESPN kuondoka kwake hakutakoma na Romelu Lukaku kwani naye pia hana nafasi katika kikosi hicho.

# Mahrez safari Arabuni imeiva

**MANCHSTER, England**

MANCHESTER City imekubali ada ya pauni milioni 30 kutoka kwa Al Ahli ili kumwachia winga wao, Riyad Mahrez, vyanzo vimeiambia ESPN.

Ofa hiyo ambayo ni pamoja na malipo ya uhakika ya pauni milioni 26 na nyongeza nyingine ya pauni milioni nne, ilikubaliwa Jumatano Alasiri.

Mahrez alipewa ruhusa na City kukosa safari ya kuelekea Tokyo nchini Japan kwa ajili ya kujiandaa na msimu mpya ili kukamilisha uhamisho huo.


Hiyo ina maana muda wa Mahrez kubakia Etihad ambapo alicheza zaidi ya mechi 200 katika misimu mitano na kushinda mataji ya Ligi Kuu England mara nne na Ligi ya Mabingwa mara moja unafikia mwisho.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Algeria mwenye umri wa miaka 32, alikuwa amebakiza miaka miwili kwenye mkataba wake, lakini alitaka kuhamia Ligi Kuu ya Saudi Aarabia.

João Cancelo amejumuishwa katika kikosi cha City baada ya kutumia kipindi cha pili cha msimu uliopita kwa mkopo Bayern Munich.

Mahrez ni mchezaji wa pili kuondoka City kufuatia mafanikio yao ya kutwaa mataji matatu msimu uliopita, baada ya nahodha i lkay Gündoi an kuamua kujiunga na Barcelona kwa uhamisho wa bure.

Bado kuna shaka kuhusu mustakabali wa Bernardo Silva, Aymeric Laporte, Kyle Walker na Kalvin Phillips, ingawa wote wanne walikuwa kwenye ndege kuelekea Japan Jumatano iliyopita.



# MINZIRO AAHIDI KUREJESHA HESHIMA PRISONS LIGI KUU

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA Mkuu wa Prisons, Fred Minziro, amesema mikakati yake ni kuona timu hiyo inacheza soka la ushindani katika mechi zote za Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo itafanyika kuanzia Agosti 15, mwaka huu.

Minziro aliliambia Nipashe amejipanga 'kuisuka' upya timu hiyo na kuondoka katika nafasi za hatari kama ilivyokuwa katika misimu miwili iliyopita.

Alisema anafahamu msimu ujao hautakuwa rahisi kwa sababu kila timu imejiandaa kuonyesha soka zuri na kumaliza kwenye nafasi ya juu.

"Mikakati yangu ni kuhakikisha timu yangu inashika nafasi za juu katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, ninaomba mashabiki wanipe ushirikiano," alisema Minziro.

Kocha huyo aliongeza katika kipindi hiki cha maandalizi ya msimu mpya, anatarajia kucheza mechi nyingi za kirafiki ambazo zitasaidia kuwaweka imara wachezaji wake.

"Nimekuta kikosi kina mapungufu machache ambayo tayari nitayafanyia kazi ili ligi ikianza kila kitu kiwe kimekaa sawa, ninaamini Prisons inayoogopewa itarejea," Minziro alisema.

Aliongeza anafahamu msimu mpya utakuwa na ushindani mkubwa kutokana na maandalizi na usajili mzuri uliofanywa na timu zote.

"Nitajitahidi tusiwe katika hatari ya kushuka daraja, tutapambana katika kila mechi, najua hakutakuwa na mechi rahisi, kila mechi kwetu itakuwa sawa na fainali," alisema kocha huyo.

Minziro amerejea Prisons akitokea Geita Gold FC ambako msimu uliopita alikuwa na wakati mzuri.



Wachezaji wa timu ya kikapu ya vijana wakifanya mazoezi ili kujiimarisha kwenye Uwanja wa JKM Park Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Serikali yataka vyama wilayani

**Na Saada Akida**

WAZIRI wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Pindi Chana, amewataka viongozi wa mashirikisho na vyama vya michezo ngazi ya taifa kusimamia vyama vyao kuanzia wilayani ili viwe imara na viandae vyema mashindano yake.

Kauli hiyo alitoa jana katika mafunzo ya viongozi wa vyama vya michezo na uzinduzi wa mfumo wa kidigitali wa usajili yaliyofanyika kwenye Ukumbi wa Kimataifa wa Julius Nyerere, Dar es Salaam.

Chana alisema viongozi wa Taifa wanatakiwa wasiangushe juhudi za Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, ambaye amekuwa mstari wa mbele kuongeza thamani katika sekta ya michezo

Alisema sekta ya michezo imepiga hatua kubwa kutokana na uongozi nzuri wa Rais Samia kwa kuwekeza katika michezo katika kila ngazi.

Aliwataka pia viongozi wa vyama vya michezo kuhakikisha wanakuwa na wanachama kuanzia wilayani ili kuwa hai, na pia kutafuta wadhamini watasaidia katika kuendesha mashindano mbalimbali.

Aliwataka pia viongozi hao kuongeza ubunifu katika kazi zao ili kuchochea hamasa na kuwavutia wadhamini.

## Yanga SC: Tutatetemesha

INATOKA UK. 24

Naye Gamondi alisema hana shinikizo lolote kuelekea msimu ujao na anaimani atafanya vizuri akiwa na mabingwa hao wa Ligi Kuu Tanzania Bara kwa mara ya pili mfululizo.

Gamondi alisema katika muda mfupi ambao amekaa na kikosi hicho, ameona wachezaji wanaojituma na kujitambua kitu ambacho kinampa matumaini ya kufanya vizuri katika kila mashindano watakayoshiriki.

"Nimezoea kufanya kazi katika shinikizo hasa soka la Afrika, mashabiki wanahitaji matokeo muda wote, kwa hiyo ni lazima ukiwa kocha ujue kuishi katika nyakati zote, ukiwa umeshinda au umepoteza," alisema Gamondi.

Kocha huyo alisema pia anaheshimu kila kilichofanywa na watangulizi wake na anatamani kufanya zaidi ya walipoishia, ndio maana ameanza mapema kukisuka kikosi hicho.

Naye Ofisa Habari wa klabu hiyo, Ali Kamwe, alisema Yanga itaendelea kutetemesha Afrika kwa kusajili wachezaji wakubwa.

"Kwa sasa Yanga imeshakuwa klabu kubwa Afrika na hata usajili tunaoufanya sasa ni wa wachezaji wakubwa, huyu (Zouazoua) ni MVP wa Ligi Kuu ya Ivory Coast, tumemsajili ili kuongeza nguvu katika kikosi chetu, kama nilivyokuwa nikisema siku zote sisi bado tuna kikosi bora ambacho hakijabadilika, tunachofanya ni kuongeza wachezaji wenye viwango vya juu na kuwafanya wachezaji waliopo wasibweteke," alisema Kamwe.

Alisema lengo wa klabu hiyo ni kufika mbali katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika msimu ujao, pamoja na kutetea mataji ya hapa nchini wanayoyashikilia.

"Kama alivyosema, hatuna masihara hata kidogo, kama kuna watu walidhani baada ya kupata mafanikio misimu miwili tutabweteka, si kweli, msimu ujao tunataka tufike kwenye ngazi za juu katika Ligi ya Mabingwa Afrika kama tulivyofanya kwenye Kombe la Shirikisho," Kamwe alitamba.

Ofisa huyo amewasisitiza wanachama na mashabiki wa Yanga kufurika katika Tamasha la Siku ya Mwananchi litakalofanyika kesho kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam ambapo watacheza mechi ya kirafiki ya kimataifa dhidi ya Kaizer Chiefs kutoka Afrika Kusini.

## Jeshi la Simba kamili Uturuki

INATOKA UK. 24

Simba itatambulisha kikosi chake kipya katika siku ya Tamasha la Simba Day litakalofanyika Agosti 6, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Katika kuanza msimu mpya, Simba itakutana na Singida Fontain Gate katika mechi ya hatua ya nusu fainali ya Ngao ya Jamii wakati fainali za michuano hiyo itachezwa Agosti 13, mwaka huu kwenye Uwanja wa CCM Mkwakwani jijini, Tanga.

# Michezo

Ijumaa Julai 21, 2023
Nipashe




## Rooney amtabiria makubwa Rice EPL

UKURASA 21

## Jeshi la Simba kamili Uturuki

**Na Saada Akida**

BAADA ya Mzambia, Clatous Chama na kiungo mkabaji mpya wa Simba, Fabrice Ngoma, kujiunga na kikosi cha timu hiyo kilichoweka kambi Uturuki, uongozi wa timu hiyo umesema ari na morali ya kikosi imeongezeka zaidi.

Nyota hao waliondoka nchini jana na tayari wameshawasili Uturuki kuungana na wachezaji wenzao katika mazoezi yanayoongozwa na Kocha Mkuu, Robert Oliveira 'Robertinho' kuelekea msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Ngao ya Jamii, Kombe la FA na mashindano ya kimataifa ya Super League na Ligi ya Mabingwa Afrika.

Akizungumza na Nipashe jana, Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema Chama na Ngoma watakuwa katika sehemu ya mazoezi yatakayofanyika leo na ujio wao umeongeza nguvu katika kambi hiyo.

Ahmed alisema kwa sasa wachezaji wa Simba wanamalizika programu ya mazoezi mepesi na sehemu ya pili ya mazoezi magumu inatarajia kuanza wiki ijayo pamoja na kucheza michezo ya kirafiki.

"Wachezaji wote watakuwapo kambini hadi kufikia siku ya Ijumaa (leo), ili kuendelea na mazoezi kulingana na programu ya Robertinho, kila kitu kinakwenda vizuri na maandalizi ya mechi za kirafiki yako katika hatua za mwisho, mwalimu anataka kuona uwiano wa wachezaji wake wote.

Lini tutacheza mechi ya kirafiki, bado sijapata taarifa rasmi lakini natambua Robertinho anahitaji kupata mechi tatu kabla ya kikosi hakijarejea nyumbani, ninaimani hivi karibuni tutapata ratiba ya mechi zetu za kirafiki," alisema Ahmed.

Aliongeza msimu ujao Simba haitakuwa na 'masihara' kwa sababu wamefanya usajili mzuri pamoja na kutayarisha jezi ambazo zina hadhi ya kuvaliwa na timu kubwa kama Simba.

"Wachezaji wote ambao tumewasajili na kuwatambulisha tayari wako kambini. Ngoma na Chama, tayari wameungana na timu na kuendelea na majukumu ya kujiandaa kwa ajili ya msimu mpya, tunatarajia kesho (leo), kufanya utambulisho wa jezi zetu na wachezaji wetu wataonekana na uzi mpya," alisema Ahmed.

INAENDELEA UK. 23




Kibegi maalum kilichobeba jezi mpya zitakazotumiwa na timu ya Simba katika msimu wa 2023/2024 kikielekea katika kilele cha Mlima Kilimanjaro ulioko Moshi, mkoani Kilimanjaro. Utambulisho rasmi wa jezi hizo utafanyika leo. **PICHA: SIMBA SC**

# YANGA: TUTATETEMESHA NCHI

●●●Yasema bado majembe mawili, yatamba furaha iko pale pale...

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

BAADA ya kumnasa kiungo, Pacome Zouzou, uongozi wa Yanga umesema umebakisha nafasi mbili ili kufunga mchakato wa usajili wa wachezaji watakaoitumikia timu hiyo kuelekea msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara pamoja na mashindano mbalimbali watakayoshiriki.

Lakini mabingwa hao wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Kombe la FA na Ngao ya Jamii, wametamba furaha itaendelea kuwapo klabuni hapo kutokana na kusajili kikosi imara.

Kikosi cha Yanga kinaendea kujifua katika kambi yake iliyoko Avic Town, Kigamboni Dar es Salaam chini ya Kocha Mkuu, Miguel Gamondi.

Akizungumza na Nipashe jana, Makamu wa Rais wa Yanga, Arafat Haji, alisema wako makini katika kuboresha kikosi chao na kwa sababu wanataka kuendelea kuwapa furaha mashabiki na wanachama wa timu hiyo kama ilivyokuwa katika msimu uliopita.

Arafat alisema wamejipanga kuboresha katika kila idara kwa kutekeleza mapendekezo yaliyowasilishwa na kocha aliyepita na Gamondi ili kupata matokeo chanya.

"Lengo letu ni kuendelea kuboresha kikosi hata baada ya usajili wa jana (juzi), bado tunaendelea kushusha vifaa, kuna eneo moja au mawili ya kuongeza watu, baada ya Zouzoua, tunaongeza mtu mwingine wa mwisho ndani ya hizi siku mbili," alisema Arafat.

UKURASA. 23


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >